# “KUKOMBOLEWA KUTOKA JEHANAMU!!”

**Ni nini kinachotendeka unapojipata katika shimo lisilo na kina na HAKUNA njia ya kurudi?!**

**Na**

**Bette L. Stevens,**
**Mchungaji/ Nabii**

**DIBAJI NA MWUNGAMO**

Shukrani zote ni kwa Bwana , aliye nipa rehema na neema na aliye uponya mwili wangu mara mbile kutokana na maradhi. Ningependa kumrudishia sifa zote na utukufu!
Pia ningependa kumshukuru mume wangu John ambaye alikuwa wa msaada sana kwangu katika uandishi wa kitabu hiki, hakika watu wengi walihitaji kusikia na kuusoma ujumbe huu. Asante sana mume wangu, Ninakupenda.
Pia namshukuru ndugu yangu katika Bwana , ndugu Patrick Kirk, ambaye ni rafiki wangu wa karibu na ye ndiye msimamizi na mtume wa Yesu Kristo. Amekuwa wa msaada sana hasaa kiroho na uongozi katika huduma!
Shukrani zingine ni kwa wawakilishi wa kambuni ya kuchapisha ya Xulon, Katara Anduze na Tracy K Sullivan,ambao walijukumika katika awamu ya kwanza ya kuchapisha kule Xulon! Asante sana kwa ujuzi wenu, utulivu, na umakini wenu katika shughuli za kuchapisha kitabu hiki! Mungu awabariki kwa utele.

Ningependa kukiri kwamba kitabu hiki hakijakua chepesi kukiandika; lakini katika yote, natumai utaelewa kuwa Jehanamu ni kweli ipo, na wacha kiwe kiamsho kwa mwili wa Kristo kwa mataifa yote, haswaa katika makanisa na huduma zilizoko Marikani.
Ninamshukuru Mungu kwa mwito huu ulio wazi kabisa wa kupeana nafasi kwa toba ya kweli!
Tafadhali kumbuka kwamba siyo mapenzi ya Mungu kwamba watu aangamie jehanamu, ila mapenzi yake ni kwamba watu wote waweze kutubu na wawe na maisha ya milele katika Yesu Kristo!
Soma; *Yohana Mtakatifu3:16-17*, hata kama hauamini, tafadhali amini inachokisema Bibilia takatifu kuhusu Jehanamu na hukumu wa Mungu.

**YALIYOMO**


| | | |
|---|---|---|
| **SURA YA KWANZA** | FATAHA | 4 |
| **SURA YA PILI** | JISAA | 5 |
| **SURA YA TATU** | MFIKO | 6 |
| **SURA YA NNE** | JELA | 7 |
| **SURA YA TANO** | KUZIMU KUPO | 8 |
| **SURA YA SITA** | YESU KRISTO MFALME WA HAKI | 9 |
| **SURA YA SABA** | VILINDI VYA JEHANAMU | 10 |
| **SURA YA NANE** | DHAMBI | 11 |
| **SURA YA TISA** | WATU WA JEHANAMU | 12 |
| **SURA YA KUMI** | ZIWA LA MOTO | 13 |
| **SURA YA KUMI NA MOJA** | KUELEWA UNYETI WA DHAMBI | 14 |
| **SURA YA KUMI NA MBILI** | TOBA YA KWELI LAZIMA IJE KILA SIKU | 15 |
| **SURA YA KUMI NA TATU** | KUFUATA DUNIA | 16 |
| **SURA YA KUMI NA NNE** | KUTAMBUA NENO LA MUNGU | 17 |
| **SURA YA KUMI NA TANO** | JEHANAMU YA MILELE | 18 |
| **SURA YA KUMI NA SITA** | MATOKEO YA DHAMBI | 20 |
| **SURA YA KUMI NA SABA** | MIUNGU YA UONGO | 21 |
| **SURA YA KUMI NA NANE** | KUFANYA UAMUZI | 22 |
| **SURA YA KUMINA TISA** | KUSHINDA KWA UKWELI | 23 |
| **SURA YA ISHIRINI** | UKWELI WA KUTOMJUA YESU: KUTENGWA MILELE NA MUNGU | 24 |
| **SURA YA ISHIRINI NA MOJA** | NI KIPI KINACHO FUATA? | 26 |
| **SURA YA ISHIRINI NA MBILI** | UHAKIKA WA JEHANAMU | 27 |
| **SURA YA ISHIRINI NA TATU** | MABADILIKO YALIYOTOKEA BAADAYE | 28 |
| **SURA YA ISHIRINI NA NNE** | UFUNUO WA KWELI | 29 |
| **SURA YA ISHIRINI NA TANO** | MAMLAKA YA BIBILIA JUU YA JEHANAMU | 30 |
| **SURA YA ISHIRINI NA SITA** | MPANGO KAMILI WA MUNGU | 35 |
| **SURA YA ISHIRINI NA SABA** | NENO LA UFUNUO WA ROHO MTAKATIFU KUHUSU BI HARUSI | 38 |
| **SURA YA ISHIRINI NA NANE** | MASWALI NA MAJIBU | 39 |
| **SURA YA ISHIRINI NA TISA** | UDHARURA WA ONO | 42 |
| **SURA YA THALATHINI** | KUSONGA MBELE | 43 |
| | KWA UFUPI | 45 |
| | KUHUSU MWANDISHI | 46 |
| | KUHUSU OVASIA | 47 |

**SURA YA KWANZA**

**FATAHA**

Haufahamu kile Mungu anawezakifanya ukijiweka wazi kwake kikamilifu na uwe na uhiari wa kutumika katika ufalme kwa utukufu wake.
Nilijisalimisha mbele za Bwana kwa mda mrefu name nikamaanisha, naye akanitumia jinzi ilivyo mpendeza.

Usidanganyike nawe uka toa ahadi ambazo hautazitimiza. Tafadhali usilivinje agano unalo lifanya na Munguambaye ni Mkuu na ahadi zake ni za milee.
Ningependa kuongezea kwa kusema kwamba kuna gharama inayo kuja na na mwito wake, kazi yake, na upako utokao kwake.
"Akawaita mkutano pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, Mtu ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike na msalaba wake, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha. Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake?
Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake?" Marko 8: 36 – 37.

Mungu anatupenda sana, lakini kwanza anahitaji utiifu wa haki kutoka kwetu, ili tuweze kuishi maisha matakatifu ndani ya Yesu na kupitia kwa Yesu Kristo.

**SURA YA PILI**

**JISAA**

Ilikuwa tarehe 19/ 4/ 2008 ambapo Mungu alinionyesha ndoto/ ono kwa ufafanuzi katika Roho Mtakatifu, jisaa kubwa ambalo mkono wake ulikuwa wazunguka kwa kasi mno, na wakati huo kukawa na mwangaza ulio ng'aa zaidi na wa amani. Katika mawazo yangu, nikamsikia Bwana akisema kwamba yu tayari kutembea. Sikulala vyema kwakuwa nilikuwa nalitazama lile jisaa.
Ninafahamu kuwa nilipoamuka ilikuwa yapata saa tisa za asubuhi; basi nilijua kwamba Bwana alikuwa aniambia kuwa ni hivyo ndivyo masaa yalikuwa yana songa kule " upande mwingine." Mkono wa lile jisaa ulizunguka kwa kasi mno!
Nilipoamka, nilimwelezea mchungaji wangu kuhusu hii ndoto/ ono ili nipate ufafanuzi kwa kuwa haikuwa ndoto ya kawaida. Ingawa mchungaji hakuilewa, Bwana alimpa mwangaza punde tu baada ya haya kutendeka. Rohoni mwangu , maneno niliyo yasikia yalikuwa "fanya hala hala, mda unakatika!"
Ingawa sikuielewa kabisa, sikuiwaza tena ndoto hii.

*"Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu" Isaia 55:8 – 9*

**SURA YA TATU**

**MFIKO**

Ilikuwa tarehe 17/ 5/ 2008; vile ninavyo weza kukumbuka, hakuna chochote kisicho cha kawaida ambacho mimi pamoja na mume wangu tulikuwa tumekitenda isipokuwa wakati mwingine tofauti ndogo ambazo ni zakawaida. Pia tulikuwa tume fanyia kazi ghala la chakula kwenya kanisa letu. Hiyo jioni tulikuwa tukiongea na mume wangu huku tukijiandaa kwenda kanisani asubuhi iliyo fuata.
Kwakuwa ninamfahamu mume wangu, mimi nilijitupa kitandani mwangu mapema ikiwa yapata saa tatu za jioni. Nilipoenda kitandani, nilisumbukana usiku ule hadi wakti wa mwisho ninaoukumbuka nikitazama saa zilikuwa saa tisa za asubuhi.
Punde tu, niliingia kwenye usingizi mnono, name nikajipata nikiteremka nikielekea chini kweny giza tororo. Kwa ghafla, nikajipata kwenye jela. Mara ya kwanza mimi sikuelewa niliko kuwa, bali ninakumbuka vilio na maombolezo na joto jingi mno! Harufu ya kiberiti ilikuwa nyingi mno nalo giza lisilo na mwisho lilikuwa limejaa kote.
Ningesikia kicheko, na nduru a uchungu. Niliviona viumbe vya ajabu, baadhi vilikuwa vyaonekana kama minyoo, vingine vina mikia na vichwa vya wanadamu. Baadaye, nilitambua kwamba viumbe hivi vilikuwa aina ya mapepo.

*“kwa kuwa vita vyetu sii vya damu na nyama, bali twapigana kinyume na ngome, nguvu na ufalme wa giza katika ulimwengu huu na uovu wa kiroho katika sehemu za juu.” Waefeso 6:12*

**SURA YA NNE**

**JELA**

Mara ya kwanza sikuweza kusonga  kwasbabu giza lilikuwa kuu mno! Sikujua niliko kuwa; bali nafahamu mawazo yangu yalivyokuwa yakitembea. Roho yangu na hisia zangu vilikuwa makini na wima. Name nikauliza “Niko wapi? Hii ni nini? Mbona sifahamu nilivyo fika hapa?”
Kasha nikaanza kutembea kidogo, nalo joto na harufu mbaya vikazidi!
Pia nikatambua kwamba mwili wangu uikuwa tu kawaida, manake kila sehemu ilikuwa tu kama kawaida. Wakayi huo nilikuwa nahisi kuwa mdhaifu kabisa.
Katika hali hii, nilipo chunguza vizuri, niliona ni kama kulikuwa na msongamano Fulani, ni kama kulikuwa na watu au viumbe vina songa . ndiyo baadaye nikatambua kuwa nilikuwa nimewekwa kwenye jela moja na viumbe Fulani. Viumbe hivi vilikuwa vikubwa mno, kisha macho yao yalini tazama kwa chuki na ghadhabu.
Viumbe hawa alikuwa nusu binadamu na nusu wanyama. Ilionekana wazi wazi ni kama mauti yyalikuwa yameningoja. Kila kiungo kwenye miili ya hawa viumbe hakikuwa sawa. Kahukuwa na kiasi katika maumbile yao.

*“Ni vipi ulivyo anguka , ewe lusiferi, nyota ya alfajiri,ni vipi ulivyo tupwa chini arthini kasha uyaharibu mataifa. Ulisema moyoni mwako, nitajiinua hadi mbinguni, nitaiinua enzi yangu zaidi ya nyota za Mungu, nitaketi juu ya milima ya makusanyiko katika kusini. Nitajiinua zaidi ya mawingu, nitakuwa kama Mungu mkuu, ilhali wewe uta shushwa chini hadi kuzimu kwenye shimo.” Isaia 14:12 - 15*

**SURA YA TANO**

**KUZIMU KUPO**

Nilipo simama na kutazama, niligundua kuwa viumbe hawa walikuwa wakinitazama kwa makini na kuwasiliana kwa njia ambayo sikuielewa.
Nikaanza kusonga mbele katika lile giza na kulionekana kan kwamba kulikuwa na handaki karibu.
Niliendelea kukisikia kilio cha watu na ilikuwa wazi kuwa walikuwa matesoni. Kisha nilisikia sauti zikiniambia: "waambie WASIJE huku chini"
Baada ya haya, kukawa na unyamavu mwingi, kasha kwa ghafla nuru kuu kabisa ikaangaza kwenye jela.
Nuru kamilifu ya bwana wetu Yesu Kristo iliyo kilamba giza chote.
Nikamwona Mwokozi Yesu, naye akanisongea na kuninyoshea mkono wake wa upendo huku mapepo yakinyamaza kwa ghafla.

Kisha nikauliza, "Mimi ni wapi?"
Naye Bwana akasema "Nina enda kukutembeza ili urudi kule na UWAONYE watu wangu. Hapa ni mahali ambapo singependa watu wangu waje! HAPA NI JEHANAMU."

*" Kwa hivyo twawasihi wapendwa, waonye walio na tabia mbovu, wafariji walio kufa moyo, wasaidie wadhaifu na muwe na subira kwa watu wote" 1 Wathesolonike 5 : 14.*

"*Watu wangu waangamia kwa kukosa maarifa: kwasababu mumekataa maarifa, name nitawakataa musiwe makuhani wangu. Kwasababu mumesahau sheria ya Mungu wenu, name nitawasahau watoto wenu." Hosea 4:6*

*"Ni mimi ndiye niliye fufuka kutoka kwa wafu, na tazama ninaishi milele, Amina, name ninazo funguo za mauti na kuzimu." Ufunuo 1:18*

*"Nikipaa juu mbinguni, wewe upo, nikikitengeza kitanda changu kuzimuni, wewe upo." Zaburi 139:8*

**SURA YA SITA**

**“YESU KRISTO, MFALME WA HAKI”**

Nili hisi kwamba nilikuwa nimesimama kando na kisha natazama juu. Niliwaona watu wanapanda wakielekea kwenye chombo kilicho onekana kuwa na shimo kubwa mno. Kisha nilitambua kuwa, mtu alipo isongea shimo hilo, liingemvuta mtu na kisha ange tumbukia ndani. Punde tu, mtu alipo tumbukia, nduru kilio na maombolezo yasiyo na kikomo yangesikika.
Nilipo tembea na Yesu, alionekana ni kama aliyafahamu yote yaliyo endelea katika mawazo yangu. Tuliendelea na matembezi yetu huku tukipita kwenye harufu kali sana ya kiberiti na joto kali. Katika harakati hizo niliyaona mahandaki ambayo yalionekana kuelekea katika sehemu tofauti tofauti.
Na ikawa kwamba kabla niliulize swali, Yesu angelijibu.
Bwana akasema, “Binti yangu, ni huku ndiko watu huenda kulingana na kiwango na aina ya dhambi.”
Nilipo chunguza karibu nami, nliona jela nyingi mno. Naye Bwana akaniambia kuwa ni huko ndiko watu huwekwa huku wakingoja hukumu yao.

Tulipoendelea kutembea, aliniambia kuwa tulikuwa karibu na kilindi cha jehanamu ya chini..
Punde tu, nilianza kuvisikia vilio vya huruma viombavyo remeha. Baadhi ya watu walikuwa wame mwona Yesu , kwahivyo walikuwa wanaomba angalau nafasi nyingine.
Naye Bwana Yesu akaniambia, watu hawa walipoishi duniani, hawakuamini  kuwa MIMI nipo, nao wakaichukulia Bibilia takatifu kuwa hadithi tu. Waliendelea kuyaishi maisha yao kwa njia walizo zipenda.
Tulipoendelea na mwendo, niliyaona machozi machoni mwa Bwana Yesu!

*“Wengi hutafuta kibali cha viongozi, bali hukumu wa mwanadamu watoka kwa Bwana” Medhali 29: 26*
*“Tazama, siku yaja, Asema Bwana, ambayo kutoka kwa Daudi, nitaliinua tawi lenye haki na mfalme atakaye tawala na kunawiri, naye ataihukumu dunia kwa haki” Jeremia 23:15*

**SURA YA SABA**

**VILINDI VYA JEHANAMU**

Yesu aliniuliza sababu ya watu kutomwamini. Bwana akasema, “Ninawapenda, nami nataka wajazwe na furaha yangu na wafurahie pamoja name!” Aliniambia kwamba Baba hukasirika watu wanapo kosa kumchukulia Yesu kwa unyeti na kumaanisha.

Tulipoendelea kutembea, ninafikiri tulifika katika kilindi cha jehanamu. Kwasababu kulikuwa na giza zaidi; huku minyoo ikiwa inatambaa juu ya watu, huku ikiwala mikono na miguu na watu wanalia na kuomboleza kwa uchungu.

Kulikuwa na mtu aliyekuwa amesimama pekeeyake, mara ya kwanza, sikufahamu kilichokiwa mkononi mwake; tulipomkaribia, tulimwona ameibeba bibilia huku akiipunga.
Yesu akaniambia kuwa mtu huyo alikuwa akihubiri injili kwenye barabara za miji na pembeni, na popote ambapo angepata nafasi; lakini alishinwa kuhubiri ukweli kamilifu na ushauri wote wa neon la Mungu!

*“Naye Yona akamwomba Bwana Mungu wake kutoka tumboni mwa samaki, akasema, nilimlilia Bwana kwaajili ya mateso yangu, naye akanisikia; nilikulilia nikiwa kilindini mwa kuzimu , nawe ukaisikia sauti yangu.” Yona 2: 1 - 2*

Tulipo endelea na safari, Yesu akaongea tena kuhusu upendo alio nao kwetu na jinzi anavyo sikia uchungu wakati watu hawataki kulisikia lolote kumuhusu na pia hawatilii maanani onyo lake kuhusu dhambi.

Punde tu, joto likawa jingi sana, name kutazama, nikaona moto ulio kuwa umewashwa na mkubwa mno. Yesu akasema, “Hili ndilo ziwa la moto”

hapa nafsi zalia usiku na mchana na zi katika mateso makuu; name nikawasikia wakimukufuru Bwana. Chuki kuu ambayo sijawahi ona ilitoka ndani mwao!
Katika sehemu hii, nilijifundisha kutoka kwa Bwana utafanyika hisia au dhambi zilizo kupeleka jehanamu. (mfano; hasira, chuki, kutosamehe, wivu, kiburi, uasi na kadhalika)

**SURA YA NANE**

**DHAMBI**

Wakati huu nilikuwa nimejawa na uoga na hofu nyingi, naye Yesu akaniambia: “Ni pamoja mawe; wala hakuna yeyoe atakaye kudhuru.” Uwepo wake ulikuwa mzuri na wakupendeza mno kiasi kwamba kinya hakiwezi kufafanua.
Kulikuwa na mchungaji mmoja wa kike ambaye Yesu aliniambia kuwa alikuwa na uhusiano wa karibu sana naye naye alimpenda Bwana Yesu sana; lakini siku moja mume wake alishiriki dhambi ya usherati. Ingawa mama huyu alikiri kuwa alimusamehe mumewe baada ya mumewe kurejea kwa Bwana na kuja kumwomba mkewe msamaha, alijaribu sana lakini moyoni hakumsamehe mumewe.
Kando na wazo kuwa alikuwa mchungaji naye alikuwa mukristo, kutosamehe kwake kulifungua mlango wa uovu wa shetani; naye binti huyu akafanyika kutosamehe, alikuwa na uchhungu mwingi moyoni, kutokana na hayo,, alipoteza upendo wake wa kwanza kwa Yesu. Binti huyu alilia na kuomboleza , kwasababu hakuwa na nafasi ya kurudi duniani.

SISTIZO: Hata jinzi tulivyo wakristo, tusipokuwa makini, tunaweza anguka na kumruhusu adui shetani kuingia.

*“Yesu akawajibu, amini amini nawambiyeni, yeyote atendaye dhambi, ni mtumwa wa dhambi.” Yohana 8: 32*

**SURA YA TISA**

**WATU WA JEHANAMU**

Kisha tukachukua mkondo mwingine, tukipokuwa tunatembea, Bwana Yesu akasuma tena, “si shauku langu kwa mtu yeyote kuangamia, bali ningependa wote wawe name mbinguni milele.”

Nilijiuliza swali mawazoni mwangu, “Mbona wanadamu wanafanya hivi?” Na ghafla, jawabu lake lijkaja

“Binti, haikufaa kuwa jinzi ilivyo; lakini dhambi ilipoingia na watu wakatofautisha mazuri kutoka kwa mabaya, ilibidi niwaruhusu wafanye uchaguzi wao. Wanao kuja hapa, ni kutokana na uamuzi wao wa binafsi; nao wakafanyika dhambi iliyo waleta jehanamu.”
Niliwaona watu wengi wakiwa wamevalila mavazi meupe, huku wanacheka, walionekana ni kama walikuwa wanasherehekea.
Yesu akasema, “Hawa ni watu walio kuwa waaminifu, walienda kanisani na kutenda kazi katika huduma zao. Baadhi yao walikuwa viongozikatika makanisa yao, lakini kiburi na kupenda pesa vikaharibu uhusiano wao nami. Walinitangaza kwa vinywa vyao ilhali mioyo yao ilikuwa mbali name.
Baadhi yao walilkuwa na roho za kuhukumu, walipokutana na wenzao, kila mara wangeongea maongeo ya kuwadunisha badala ya kuwaonyesha upendo wa AGAPE. ”

*“Na kwa malaika wa kanisa la Laodesha, yaandike mambo haya, na wale washahidi waaminifu tangu mwanzo wa uumbaji waseme Amina. Ninayajua matendo yenu, ninyi hamuko baridi wala moto, musipokuwa baridi au moto, nitawatema kutoka mdomoni mwangu. Kwasababu mwajitajirisha wala hamukosi chochote; wala hamutambui kuwa mu holela, wahitaji, masikini, vipofu na uchi ……….”*
*Ufunuo 3:13 - 17*

**SURA YA KUMI**

**ZIWA LA MOTO**

Tuliendelea na mwendo, ingawa tulilikaribia ziwa la moto, tuligeuka tukachukua mkondo mwingine naye Yesu hakunena lolote kuhusu ziwa la moto. Nili tambua kwamba kulikuwa na harufu nzito sana ya kiberiti nalo joto lilikuwa kuu mno; watu walilia na kusaga meno huku wakimudhihaki na kumukufuru Roho Mtakatifu.
ningehisi chuki, wivu na kiburi vikidhihirika ndani mwao. Nilipo mtazama Bwana niliyaona machozi yakitiririka kutoka machoni mwake, kabla sijakifungua kinywa change kunena lolote, Yesu alijibu kwasababu aliyajua maswali yote hata kabla niyaulize.
Yesu akasema, "Binti yangu, Dhambi zote ambazo ni nyeti sana zimewakilishwa kwenye ziwa la moto. Dhambi hizi zikiwemo; Uovu, kiburi, kuropokwa, kumukufuru Roho Mtakatifu, roho za udini na uelekezi, na kukosa toba ya kweli. " aliendelea na kusema "Ziwa la moto ni kali mno, na lina lamba!"
Nami nnikaw ninajiuliza, "NI kitu kipi kitakacho fuata?"

*"Nayo mauti na kuzimu vilitupwa kwenye ziwa la moto. Haya ndiyo mauti ya pili. Na yeyote ambaye jina lke halikupatikana kwenye kitabu cha uzima cha mwana kondoo pia alitupwa kwenye ziwa la moto" Ufunuo 20 : 14 – 15*

*"Bali waoga a wasioamini, waovu, wauaji, na wachochezi, na washirikina na waongo wote watatupwa kwenye ziwa la moto na kiberiti, haya ndiyo mauti ya pili." Ufunuo 21:8*

**SURA YA KUMI NA MOJA**

**KUELEWA UNYETI WA DHAMBI**

tulipo endelea kutembea uwepo wa Bwana ukwa mzito sana , naye akageuka na kuniambia, “ Mimi ndiye niliye zitwaa dhambi zote ili watu waishi name milele!” katika harakati hizo, mapepo yalipiga kelele yakilia, huku tukiwa tunaondoka kwenye ziwa la moto, joto na harufu ya kiberiti iliendelea kuyachoma mapua na macho yangu kwa sababu joto lilikuwa kali na harufu ilikuwa nyingi mno.
Nami nikauliza, “” ni kwanini watu wengi hawaamini ndani yako?” Naye akajibu, “ Binti yangu, watu wengi wameichagua dhambi badala yangu: Kunao wengi sana wanao penda wanadamu wenzao sana na hata wamawafanya miungu badala yangu. Ni Kwa huzuni sana kwambaq wamejiingiza kwa uchawi, kiburi na oungo; ambavywo ni uasi kwangu. Wao wanafikiri ni saw asana kuyafanya mambo haya, lakini chanzo cha hayo yote ni mawazo; shetani huyashambulia mawazo na hisia zenu ili apate nafasi ya kuingia. “ Aliendelea na kusema, “Kwa miaka mingi sana watu wamefundishwa kuhusu Neema na Rehema. Hiyo ni sawa kuvifanya vitu hivi; na kisha waje kwangu na moyo nusu kutafuta faraja, na kisha wana tubu wakati hali inawaruhusu. Hii ni sawa na kuikanyagia DAMU yangu chini ya miguu yao! Hakuna neema iliyo na gharama ya chini, hebu nikueleze, iwapo watu hawa hawatatubu kwa haki, hawataingia kwa ufalme! Ninapo kurejesha huko, Kumbuka KUWAONYA na uwaambie watu wangu kuwa mda ni mfupi kuliko vile wanavyo fikiria. Maonyo baada ya megine yameletwa na manabii wangu, nao wameyaasi. Hata hivyo, usikate tama juu yao, endelea kuomba huku ukitoa mlio wa tahadhari, na hukumu itaendelea kuongezeka. Sasa nime kuambia haya mambo usipigwe na mshangao utakapoyaona yakija kutimia.”

Tuliendelea na matembezi yetu katika upande mwingine, kando na ziwa la moto, kulikuwa na vyumba ambavyo vilikuwa ni jela. Kila chumba kilikuwa na mtu ndani huku kila chumba kikiwa na pepo mmoja anayeichunga.
Tulipopita, mapepo yalitoa sauti, yakitema huku yakiwa yabnatutazama kwa ghadhabu na chuki.

SISTIZO: Tafadhali jua kwamba, kukosa kumuamini Mungu, na kukosa kuamini kile anacho kisema atatenda ni sawa na kumuasi Mfalme wa wafalme!

*“Kunavyo vitu sita ambavyo Bwana anchukia, Nam, vitu saba ambavyo ni chukizo mbele zake: Majivuno, Ulimi ushuhudiao uongo, Mikono imwagayo damu isiyo na hatiya, Moyo unao panga uovu, miguu ikimbiliyayo uovu, Mshuhuda wa uongo na Yule apandaye mmbegu ya chuki katikati ya wapendwa.”*
*Medhali 6:16 – 19*

Ninaomba nikome hapo kwa kusema kwamba Mungu anaupenda wote, na kwa huu upendo mkuu ametoa onyo.
Jinzi vile mzazi anavyo toa onyo kwa wanawe, vivyo hivyo, Mungu kwa uaminifu anawaonya wanawe.

*“Kwa kuwa imewekwa kwa mwanadamu kukufa maramoja, kisha baada ya kufa ni hukumu”*
*Wahebrania 9: 27*

*“Kwa kuwa wakati umewadia ambapo hukumu unaanza atika nyumba ya Mungu, iwapo waanza nasi, itakuwa vi[pi kwa wale wasio iamini injili ya Mungu? Na iwapo ni wenye hali wachache wataokoka, wenye dhambi watasimama wapi?” Waraka WA Petero wa kwanza 4: 17 - 18*

**SURA YA KUMI NA MBILI**

**TOBA YA KWELI LAZIMA IJE KILA SIKU**

Tulitembea kwenye handaki linguine lililoonekana kuelekea upande wa kulia. Handaki hili lilikuwa na jela nyingi kabisa katika pande zake kiasi kwamba singeweza kuzihesabu.
Bwana Yesu akaniambia kuwa kuzimu yaendelea nakuendelea, bila kikomo. Naye akasema kwamba mradi nafsi imeingia huko, haina njia ya kurejea tena.
Wakati hou nizisikia nafsizikilia kwa huruma na uchungu wa mateso. Nilihisi kuzidiwa sana na hali hiyo amabyo nafsi zilikuwa zikipitia. Ni wazi kwamba tulikuwa vado karibu na ziwa la moto. Tulikuwa katika mwendo wa kasi sana, name ninaaamini kuwa Bwana Yesu alikuwa akinibeba kwa sababu mahali tulipokuwa kuliogofya sana.
Tulipoendelea na matembezi yetu, Bwana aliniambia kwamba yamuhuzunisha sana wakati ambao wanadamu hawamuchukulii kwa umakini na unnyeti. Ingwa ashaa dhibitisha ukuu wa upendo wake kwa kila mmoja, lakini alinisisitizia kuwa: DHAMBI ni DHAMBI, iwe ndogo au kubwa.
Ilikuishi maisha matakatifu, ni lazima tu dumu uweponi mwake kwa sifa na kuabudu; tulisome na kulitii neon lake kila siku; tuwe na toba ya kila siku, turejee kwa upendo wa kwanza na tumtafute kwa bidii.

*“vivyohivyo ninawaambieni kuwa kunayo sherehe mbinguni mwenye dhambi mmoja anapo tubu, kuliko wenye hai tisini na tisa ambao hawahitaji toba. Luka 15: 7*”

**SURA YA KUMI NA TATU**

**KUIFUATA DUNIA**

Kipindi kilicho fuata, nilimwona mtu anaongea huku akitembea, anasonga mbele na kurudi nyuma. Ilionekana kanakwamba kulikuwa na jukwaa kubwa, nalo lilikuwa limefunikwa na mkeka wa rangi ya samawati huku kukuwa na viti vizuri kabisa vikiwa vimewekwa.
Name nikasema, “Mbona sielewi anachokifanya mtu huyu?”
Yesu akanijibu na kusema, “mtu huyu alikuwa mchungaji na vilevile mwalimu wa neon. Mchungaji huyu alipo anza kazi ya huduma, angelienda na kumsaidia kila mtu, naye angetoa kile alicho kuw nacho iwapo uhitaji ungepatikana. Angelihubiria kila mtu yeyote ambaye angemsikiliza. Aliamini kuwa maisha yake yalikuwa sawa , naye alikuwa na utoshelezi kwa sababu alimpenda Mungu, tena alipenda kufundisha.”
Nami nikamwuliza Bwana kilicho msababisha mchungaji huyo kuambulia huko.
Yesu akasema,”Miaka ilipo endelea na huduma ukakuwa, pesa ziliongezeka naye angekinunua chochote alicho kihitaji kanisani, vitu kama; jingo nzuri, mkeka, viti bora zaidi n.k. na vitu kivyo vikawa bora zaidi kumliko Mungu. Alianza kuyaishi maisha “mazuri” wala hakumhitaji Mungu tena, hata hivyo, vitu hivi vyote havikumpatia furaha na amani”

*“kwa hivyo, kando na kanuni za mafundisho ya Kristo, wacha tufuate ukamilifu, wala sio msingi wa toba kutokana na matendo maovu nay a imani kumwelekea Mungu” Wahebrania 6: 1*

*“Kisha Elija akaja na kuwaambia, ni kwa mda gani mutaendelea kubishana kwa mambo haya mawili, iwapo Bwana ndiye Mungu, basi mfuateni, vivyo hivyo iwapo ni baali, mfuateni.” Wafalme wa kwanza 18: 21*

Baali ni ulimwengu.

*“iwapo ni uovu kwenu kumtumukia Bwana, basi mchaueni leo mtakaye mtumikia; iwapo ni miungu walizo zitumikia baba zenu ng’ambo ile nyingine, au miungu ya waamori ambao tumemiliki nchi yao. Bali mimi na nyumba yangu nitamtumikia Bwana.” Yoshua 24:15*

*“Hakuna awaye yeyote awezaye kuwatumikia mabwana wawili, kwasababu itamlazimu kumchukia mmoja kasha ampende mwingine; la sivyo, atamwamini mmoja na kumdharau mwingine. Huwezi ukamtumikia Mungu na pesa.” Mathaye 6: 24*

**SURA YA KUMI NA NNE**

**KUTAMBUA NENO LA MUNGU**

Katika yale matembezi, nikamwona mwanamkw mmoja aliye kuwa na nakala kadhaa za bibilia mezani. Alionekana kana kwamba ananukulu maandiko, na pia alionakana ni kama alikuwa akijiaandaa kupeana ujumbe.

Kulikuwa na watu wengi sana hapo waliokuwa wakilia, wakipiga nduru na kusaga meno. Nao walikuwa wakilia na kusema kuwa hawakutaka kuwa kuzimuni. Ilikuwa ya kutisha sana kuona nafsi zao katika mateso yasiyo na kikomo na pia kujua kwamba walikuwa jehanamu umilele wote.

Yesu akaniambia, “Watu hufundisha na kuongea juu yake, lakini inapofika kwa upande wa kujitoa kikamilifu na kuwa na uhusiano wa karibu na kuwajibika kulingana na neon la Mungu, wao huondoa na kutotenda sehemu ya neno. Jinzi vile mimi Yesu nilivyo MFALME na HAKIMU mtakatifu, wao hutoa unabii, wananena na kunena kwa ndimi, wala hawayasalimishi maisha yao kwangu kwa ukamilifu.”

*“Soma na ujionyeshe umekubaliwa mbele za Mungu na mfanyikazi asiye aibikia injili, anaye ligawa neno la ukweli sawasawa.” Temetheo wa pili 2: 15*

*“Musimuzime Roho Mtakatifu” Wathesolonike wa kwanza 5: 19*

Swali: Je wewe ni mpendeza Mungu, unaye mfuata Mungu na kusimama katika neno bila kukubaliana na uovu wala hila?

Au

Je wewe ni mpendeza mwanadamu uliye na mguu mmoja duniani kasha mwingine kanisani?

**SURA YA KUMINATANO**

**JEHANAMU YA MILELE**

Kufika hapa, ilikuwa wazi kwamba kila nafsi ilikuwa inateswa zaidi yanufahamu wowote wa wanadamu. Niliangalia karibu name wakati harufu ya kiberiti ilikuwa nyingi mno, huku joto likiwa jingi zaidi na zaidi. Mapepo nayo yakiwa mengi ingawa hayakusongea karibu zaidi lakini yalipiga kelele wakati wote. Baadhi ya mapepo yalikuwa ndani ya jela ingawa kulikuwa na mapepo ambayo yamepewa kazi kuchunga kila chumba. Mapepo yaliyokuwa pembeni yange toa sauti ya kuogofya na kupigia kelele nafsi zilizo ingia huko kuzimu. Nao hao mapepo walizimbusha nafsi zilizo fika huko dhambi zilizo sababisha wakenda huko.
Mapepo yaliyokuwa ndani ya vyumba yalitafuna vitu vilivyo onekana kama minyoo na nyama.
NAYO MAMBO HAYA YALIENDELEA USIKU NA MCHANA BILA KIKOMO!!
Tena Yesu akanikumbusha kwamba jehanamu ni ya milele, na hayo mateso na kusaga meno ni milele na milele. Niliwaona baadhi ya watu walio kuwa wamefungiwa kwenye jela wakiyasaga meno yao, hata baadhi yao wakijaribu kuya ng'oa.
Ninafikiri Bwana Yesu alijua kwamba singevumilia zaidi kwasababu jehanamu ni kubaya sana na kwaogofya mno.

SISITIZO: Najua kila mara kunayo maswali kuhusu jehanamu inavyo onekana. Wacha niyaseme haya, nafsi inapoanza keunda huko, kunaonekana nu kama mahalipa kutembea tu, ila kunayo hii ndege kubwa ya hewa inayovuta na kumeza na kumeza mtu. Mradi tu mtu anapofika kule ndani, yeye hufungiwa kwa jela. Wakati mwingine kuna mapepo ndani ya hizo jela , lakini kuna mmoja ambaye ni mkubwa anasimama nje wakati wote.
Jela hizi zinaye milango ya chuma. Huko kuna giza wakati wote nayo mateso ya nafsi ikiendelea wakati wote.
Nfsi zingejukunja na kulia, mapepo nayo yangeenda na kuzigonga nafsi hizi na kuzipigia kelele usoni. Aina hii ya mateso kwa nafsi haina kikomo
Unapoendelea kuingia jehanamu zidi, joto nalo linazidi, na makali ya kilakitu yanaongezeka.
Yafaa tukumbuke kwamba Jehanamu haina mwisho, kunayo mahandaki tofauti tofauti mbazo ndizo njia kule jehanamu. Sidhani kama Bwana alinitembeza katika kila sehemu kule jehanamu. Lakini ningependa kukueleza kwamba uzito wa dhambi zako una kirimia utakapopelekwa kule jehanamu,baada ya kutolewa kwenye jela.
Yeli aliniambia, "Ziwa la moto limo kwenye giza tororo kwa sababu ya asili ya dhambi ambayo nigiza." Najua kuwa tulipokuwa karibu na ziwa hilo kulikuwa na wengi walio kuwa wakimukufuru Roho Mtakatifu. Maongezi mengine machafu naya aibu ilitoka vinyani mwa wale waliokuwemo ziwani.

Mapepo yangkusanyika na kuzitwaa baadhi ya nafsi na kuanza kuzitigiza kwa fujo mno. Iwapo umewahi kuwa katika hali ambayo wamona mtu anaongea na kuongea zaidi na zaidi bila hat ishara ya kunyamaza mpaka unnahisi umasinyika, hivyo ndivyo mambo yalivyo kule jehanamu. Kunazo kelele za kilio, maombolezo na mateso yanayo shitua moyo na ambyo hayawezi kuelezeka wakti wote , usiku na mchana bila pumziko huku mapepo yakiweko nyakati zote.
Yesu akaniambia, "Kila mara mapepo hutaka kuleta kumbukumbu la dhambi zote zilizo pita."
Joto lilikuwa jingi sana, lina choma, nacho kiberiti hakikomi kuwaka kwasababu ya dhambi zilizomo jehanamu.
Yesu akasema, "Dhambi zote ni harufu mbaya mapuani mwangu." Kasha akanikumbusha kwamba bado anampenda kila mmoja na kila mtenda dhambi ingawa hawauitikii upendo huu kwa kumpenda.

Aliendelea kuniambia kuwa TOBA yafaa kuwa tendo la kila siku kwasababu mwanadamu bado anaishi duniani ambako dhambi ni nyingi kutokana na muanguko wa mwanadamu.
Shetani amewadanganya wengi sana kiasi kwamba hawawezi kutambua.
Kwahivyo, (mkiisikia sauti yake leo, msiifanye mioyo yenu kuwa migumu na kumkasirisha Mungu jinzi mababa zenu walipo nijaribu kule jangwani nao wakishuhudia kazi yangu kwa miaka arobaini. Hivyi mimi nilikasirishwa na kizazi hicho kwakuwa alitenda dhambi mioyoni mwao wala hawakuzifahamu njia zangu. Kasha nikaapa moyoni mwangu kwamba wasione pumziko). Iweni waangalifu kwamba asiwemo kati yenu aliye na moyo muovu wa kutoamini, na kumwach Mungu aishiye.
Twafaa kujua kwama katika maandiko haya matakatifu, Mungu yu anena kuhusu kuto amini kwa wana wa Iasrali.
Pia kuna onyo hapa kwetu sisi waumini wa sasa tunaomkiri Yesu Kristo, “ Msiifanye mioyo yenu kuwa migumu,na msiondoke kwa njia za Mungu, ambalo ndilo tendo la kukusudia kuondoka na kuwacha ufunuo wa Bwana na mapenzi yake!”

Watu wengu wameuwacha upendo wao wa kwanza (Yesu Kristo); nao wamekataa kudumu katika mafundisho timamu ya neon lake takatifu. Mioyo yao imafanywa migumu nao wanamtafuta Mungu kwa uchache.
Nasi twasahau kwamba Mungu yu atuhitaji sisi wote!

*“Siku hiyo wengi wata niuliza: Bwana, Bwana, situlitabiri kwa jina lako na kufukuza mapepo kwa jina lako na kutenda miujiza kwa jina lako? Nami nitasema, siwajui, ondokeni enyi watenda dhambi.” Mathayo 7: 22 - 23*

**SURA YA KUMI NA SITA**

**MATOKEO YA DHAMBI**

Tulipoendelea na matembezi, Yesu alikimya kwa mda, name nikataka kuuliza swali kwasababu unyamavu huu ulikuwa wa kitofauti. Harusu ya kiberiti ilizidi tena. Kungesikika tu sauti ya moto unao lamba! Kiwango cha mateso kilikuwa kuku sana na kisicho na huruma.
Nilipotaka kutoroka, Yesu akayajua mawazo yangu kasha akaniambia, "subiri, hakuna chochote kitakacho kuumiza."
Nikamuuliza, "Je, tuko sehemu tofauti?"
Akani jibi, "Nam, tuko upandu mwingina wa ziwa la moto. Nataka nikuonyeshe kitu."
Ilionekana kana kwamba tulipita kwa njia iliyo kuwa nyebamba. Tulipo songa karibu, nilimsikia mtu akicheka. Nilipo tazama vyema, nilitambua kwamba kulikuwa na watu kadhaa katika sehemu hii. Niliwaona wanaume wawili na wanawakw wawili; name nikahisi kuwa mambo hayakuwa sawa.
Walipomwona Yesu, walianza kuchafya, kutema mate na kumpigia kelele huku wakimnenea mambo ya aibu.
Mmoja wao alilia kwa uchungu sana huku akipiga kelele akisema, "tafadhali nipe nafasi nyingine, sikujua kwamba nitakuja huku. Tafadhali nisaidie!"
Machozi yalionekana tena machoni mwa Yesu, kasha nikataka kumwomba Yesu kwamba turudi huko iliniweze kumsaidia Yule aliye kuwa akilia;
Lakini akasema, "Usiwahi tazama nyuma."
Bwana aliniambi kuwa watu hawa alichaguwa kile walichotaka kukifanya, wala hawakutaka chochote kumuhusu Yesu walipokuwa duniani. Baadhi yao walifikiria kuwa yesu ni hadithi tu. Ingawa bibilia ilifundisha kuhusu dhambi hizi, wao waliendelea kwa njia zao. Kwahivyo walikuwa wamejawa na chuki na uchungu kumwelekea Yesu. Nafsi ile iliyokuwa ikilia ilikuwa na maisha mema duniani; lakini alikututana na mtu aliyemfanya aingie dhambini. Alikuwa amemwamini Yesu lakini alikuwa anamtafuta mtu mwingine tofauti na mpya. Hakuwahi jua kwamba angeambulia jehanamu, hata hivyo alikuwa ameokoka kanisani miaka mingi na hata alikuwa amebatizwa. Yeye alifikiria kwamba alikuwa sawa kwasabau hakunywa pombe wala kuvuta sigara. Alichukia moshi wa sigara, naye aliilinda familia yake vyema kabisa naye angeenda kanisani mara moja baada yam da mrefu.
Alipenda muziki kwa sababu ingemfanya asikie kulia, na watu kanisani mwake walikuwa na mtindo wa kuvaa; naye aliwafaamu vyema kabisa marafiki wake na akaupenda ushirika.
Kila mara kungekuwa na ghafla yoyote, angepate mahali pa kuingia na kutumika, hii ilikuwa ni starehe nzuri maishani. Lakini unyeti wa dhambi zake ulimsababisha achomwe jehanamu milele.

*"Hakuna mwanadamu yeyote awezaye kutumikia mabwana wawili, itampasa amchukie mmoja na kumpenda mwingine, au atamuheshimu mmoja na kumudharau mwingine. Huwezi kumtumikia Mungu na pesa." Mathayo 6:24*

*"Mwana wa Adamu atawatuma malaika wake, nao wata vikusanya vyote ambavyo ni chukizo na uovu katika ufalme wake na kuzitupa kwenye tanuru la moto. Kutakuwa na kulia na kusaga meno." Mathayo 13: 41 -42*

*"Ni hi vyo ndivyo itakavyo kuwa mwisho wa dinia, malaika watkuja na kuwatenga wenye dhambi kutoka kwa wenye haki, nao wenye dhambi watatupwa kwenye tanuru la moto. Kutakuwa na kulia na kusaga meno." Mathayo 13: 49 - 50*

**SURA YA KUMI NA SABA**

**MIUNGU YA UONGO**

Tulipo endelea na matembezi, kuna kivuli kilichosababisha nikageuka. Kunayo jamii iliyokuwa kanisani kwa mda mrefu sana. Kwa miaka hii yote, walihudhuria mkutano kwa uaminifu, na kila mara walikuwa na uhiari wa kusaidia. Pia walikuwa waalimu wa shule ya jumapili. Walikuwa wamefanya kazi na kustaafu wakiwa na hela kwenye benki na watoto wao walikuwa wakubwa.
Walitaka kufanya kazi zaidi kanisani, nao wangepatikana kila siku. Ingawa pia walitaka kusafiri na kuhubiri katika sehemu zingine. Walikuwa na kiwango kizuri cha hela kwenye benki na kasha wakakatiza kwenda kanisani. Walienda kila walikotaka nao wakayafurahia maisha mazuri katika Kristo, nao wakatukia maishani. Walitaka kuwasaidia watu, lakini wakawa na shugulinyingi sana.
Fedha zilikuwa zimegeuka kuwa "mungu" wao, na haungewasikia wakiongea kumhusu Yesu wala kumrudishia utukufu kwa vile vyote walivyokuwa navyo. Walikuwa na boma nzuri sana na kiwango chao chao cha maisha kikawa ch juu sana. Kila mara walipenda kutambulika popote walipoenda, walipotoka kabisa kutoka kwa Mungu. Walivitegemea vitu vya asli ambavyo maisha yangewapatia.

KUMBUKA: Ya faa tukumbuke kwamba kiburi na kupenda fedha ni aina ya uasi mbele za Mungu na wala havitatufikisha kwa ufalme wa Mungu.

*"Pia yeye apokeaye mbegu katika miiba ni yeye anaye anayelisikia neno na kasha shughuli za dunia na udanganyifu wa utajiri unaua neno, na kasha mtu anakosa kuzalisha matunda." Mathayo13:22*

*"Je, hamjui kuwa watendadhambi hatauridhi ufalme wa Mung? Musidanganyike, wasinzi, waabuduo sanamu, washerati, waongo, wanaotumia miili yao vibaya, wezi, watamaa mbaya, walevi, wachochezi wote hawatauona ufalme wa Mungu." Wakorintho wa kwanza 6: 9 – 10*

*"Kisha Yesu akawaambia wanafunzinwake, amini amini nawaambieni, itakuwa vigumu kwa tajiri kuingia kwa ufalme wa mbinguni. Nawaambieni tena kuwa, ni rahisi kwa ngamiakupita kwa tundu la sindano kuliko tajiri kuingia kwa ufalme wa mbinguni." Mathayo 19: 23 – 24*

*"……………… ni heri kutoa kuliko kupokea" Matendo ya Mitume 20: 35 b*

**SURA YA KUMI NA NANE**

**KUFANYA UAMUZI**

Yesu akaanza kutembea pamoja name, sikujua la kusema. Kulikuwa na mambo mengi sana niliyokuwa nimeyaona, name nilitaka tu niondoke, niende mahali tofauti ili nianze kulia.
Mara tena Yesu akawa ameyafahamu mawazo yangu, naye akasema, “Binti, hii ndiyo maana mambo hayo yote umeyaona, ni lazima wende uwaelezee watu wangu, bado hawajaelewa kwamba mambo yanayo onekana sawa kwa macho yao ni dhambi. Yaumiza moyo sana, na tena yamuumiza babangu kuwaona watu wangu, ambao wamehaidi kunipenda na kunitumikia wametengenezea dhambi mwanya. Wanafaa kunitafuta, name ni Mungu mwenye wivu! Ni lazima wageuke kutoka Dhambini na watubu. Waambie watu wangu kuwa wanafaa kuchukua mda zaidi name. wanafaa kunitafuta na kutubu kila siku. Mimi ninawapenda, lakini wao wame wamegeuka kutoka kwangu, wameruhusu mambo ya dunia hii kuwa miungu yao.”
Baadhi ya watu husema, “Tazama yale ambayo Bwana amefanya.” Ilhali mioyoni mwao wanajitwalia utukufu wala si Mungu.
Ayesu akasema, “Kunao wengine ambao wamefanya fedha kuwa “mungu” wao, nao wanafanya kazi kwa nguvu sana kuhifadhi hizo fedha, huku wakiziita vitu vyao. Ilhali Hizo si njia zangu, kwasababu wanajipenda wao wenyewe na fedha zao. Watu hawa wanamtumikia Mungu wa uongo na pesa.”

*“Na kwa malaika wa kanisa la leodesha, yaandike mambo haya na waaminifu na washuhuda wa kweli waseme amina, tangu mwanzo wa uumbaji. Nayajua matendo yenu, ninyi hamko moto wala baridi, ni heri mungelikuwa moto au baridi. Kwasababu hamna joto wala baridi, nitawatema kutoka kinywani mwangu, kwasababu mwasema ninyi ni matajiri wala hamuhitaji chochote, wala hamufahamu uovu wenu, na uhitaji, na umaskini, na upofu na uchi wenu. basi nawashaur kwamba muinunue dhaabu iliyo pitishwa motoni kutoka kwangu ili muwe tajiri, na vazi jeupe ili muvishwe na uchi wenu ufunikwe. Na macho yenu yatiwe mafuta ili yaweze kuona.*
*Waleninao wapenda, ninawakemea na kuwaadhibu. Kwahivyo chocheweni na mutubu. Tazama nasimama mlangoni na kubisha, yeyote atakayesikia sauti yanguna aufungue mlango, mimi nitaingia ndani, name nitakula naye , naye atakula name.” Ufunuo 3: 14 - 20*

**SURA YA KUMI NA TISA**

**KUSHINDA KWA UKWELI**

Yesu akanipeleka sehemu nyingine iliyokuwa mbali kidogo na ziwa la moto. Sijui hasa upande wa jehanamu tulipo kuwa, lakini Yesu akanionyesha mishororo mingi ya vyumba ambavyo ni jela ambavyo havingeweza kuhesabika.
Niliwaona watu wakielekezwa kwenye vyumba hivyo wakipitia njia iliyo kuwa nyebamba.
Ilikuwa ajabu kwasababu ningesikia manong'ono na mateso. Baadhi ya mapepo yalikuja na kujaribu kunishika, lakini mapepo makubwa yalikuja na kuwavuta wake wadogo kutoka kwangu na kasha wangewachekelea na kuwadhihaki. Mapepo hayakukuwachila kilio cha maombolezo.
Nyagonyago na kilio cha huruma kiliendelea bila mwisho. Hapo nikatambua kwamba mapepo yalifurahia kuzitesa nafsi zilizo hukumiwa kwa kuwaletea kumbukumbu la dhambi ambazo nafsi zilitenda, huku nafsi zikikumbuka mabo waliyo yanena wakati walikuwa bado duniani, wala nafsi hizi hazikuruhusiwa na mapepo kutulia.
Yesu alikuwa ame nyamaza kwa mda , name pia nilikuwa nime kimya , Yesu alipo fungua kinywa chake kunena, aliniambia kuwa kulikuwa na watu hapo walioambiwa kumuhusu, nao waliijua injili, waliyajua maisha ya Yesu na kifo chake, wala hawakukubali uhusiano wowote na ye.
Kulikuwa na kuchanganyikiwa kwingi sana hadi wakafikiri walikuwa na mda mwingi wa kujirekebisha. Baadhi yao walifikiri kuwa walikuwa sawa kwasababu ya huduma walio kuwa wakitoa, ingawa baadhi yao walikuwa wameokoka wakati mmoja maishani, kwasababu ya ushawishi wa dhambi walirudi nyuma na kuzitenda dhambi za awali. Kwahivyo, kwasababu ya wokovu waliokuwa nao wakati mmoja, hata baada ya kutenda dhambi, walijidanganya kwamba walikuwa sawa kiroho.

NAKILI: Watu wengi hufikiri kuwa mradi wameokoka, basi imetosha. Lakini kwasababu ya mawazo ya kujidanganya na mafundisho potovu, nafsi hizi zaangamia jehanamu milele.
WOKOVU katika toba kamili ni ufunguo wa kumleta mtu katika

Uhusiano wa ndani, na Mungu kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo anayetusamehe dhambi zetu kupitia kwa toba ya kila siku.

*" Yeye alituokoa katika nguvu ya giza, akatuleta salama katika ufalme wa Mwanae mpenzi, ambaye kwa njia yake tunakombolewa, yaani dhambi zetu zinaondolewa" Wakolosai 1: 13 - 14*

*" Nawaambieni hakika sivyo; lakini nanyi, hali kadhalika, msipotubu, mtaangamia kama wao" Luka 13: 3*

*" Mungu alifanya kama kwamba haoni nyakati zile watu walipokuwa wajinga. Lakini sasa, anaamuru watu wote kila mahali watubu. 31 Kwa maana amekwisha weka siku ambayo atauhukumu ulimwengu kwa haki kwa njia ya mtu mmoja aliyemteua. Mungu amewathibitishia wote jambo hili kwa kumfufua mtu huyo kutoka wafu!" Matendo ya Mitume 17: 30 – 31*

**SURA YA ISHIRINI**
**UKWELI WA KUTOKUMJUA YESU: KUTENGWA MILELE KUTOKA KWA MUNGU**

Tuliendelea na matembezi yetu, ingawa nilikuwa nimenyamaza, lakini nilijifundisha mengi. Yale niliyoyapata katika roho yalikuwa yamenizidi na uzito wake kiasi kwamba singeweza kueleza.
Yesu akasema, “Ni wakati wako kurejea huko, lakini kabla ya hiyo, habu nikufrahishe kidogo na haya!”
Tulipoendelea, mapepo yalionekana kutulia nalo giza lilikuwa tororo mno, na katika giza hilo, Yesu akasema, “wajua jinzi ninavyo kupenda binti yangu, lakini punde tu, sitakuwa nawe.”
Punde tu, Nikapiga kelele, “Yesu?!?!?! Yesu?!?!?!” na punde hakuwepo tena, name nikajipata pekee yangu. Kilichofuata, nilijipata kwenye jela huku kukiwa na giza tororo vikiwa vmenibana.
Kisha hiyo harufu buvu, malalamiko yasioyo na kikomo, pamoja na kilio cha kuhurumisha. Nilirudi na kulala kwa kile chumba kanakwamba ninakufa. Kasha mapepo wawili wakanijia, vichwa vyao havikuwa na umbo sawa, na vilionekana kama vichwa vya aina Fulani ya wanyama. Miili yao ilionekana kama ya waanadamu ingawa ilikuwa kombo. Kitu kilipita kati yao, na hayo mapepo yakasema,
“Yesu hayupo sasa.”
Punde tu, nikajipata nimesahau ufahamu wangu kwa Yesu, wokovu, na tumaini la utukufu wa mbinguni. Mapepo hayo yalinishika na kunitupa kwa fujo kwenye sakafu ya jela, nilihisi upweke na uchungu mwingi ulionisababisha nikapige nduru kwa sauti yangu yote, punde tu, nikamwona Yesu kando yangu. Mara tena nikapokea kumbukumbu kamili la Bwana Yesu kwamba yeye ndiye tumaini letu la wokovu na msamaha wa dhambi, naye ndiye njia ya pekee ya kuliepuka ziwa la moto.
Punde tu, uchungu ulipotea Yesu alipo nitwaa kutoka sakafuni.
Nilijawa na furaha sana nilipojipata nimeondoka kwa yale mateso na nimo kwenye mikono yake ya upendo.
Kufika hapa, Bwana Yesu aliniambia mambo mengi ambayo aliniambia niliambie kanisa na huduma zote na kwa kila Bibi Harusi kutoka kwa mataifa yote wa Bwana wetu Yesu Kristo.
Ni muhimu sana kwetu kuelewa kwamba Yesu hataki mtu yeyote aangamie jehanamu. Na watu wakienda huko ni kutokana na matendo yao maovu ambayo wanachagua kuyafanya Na kukubaliana na vitu za kiroho! Jehanamu ni hakika na kilakitu ni hakika jinzi ambavyo imeelezwa kitabuni humu.
Tuwe tumeudhika kwasababu ya ukweli wa Mungu, au tumekataa kuamini, ukweli unabaki kwana tunajua jukumu la siku za mwishoambalo tumepewa na Mungu, kwamba tutubu kila siku. Iwapo tutakosa kutii na tupuuze ama tuasi jukumu hili kuu la TOBA ya KILA SIKU, tutakuwa katika hatari ya kuambulia kwenye moto wa jehanamu.
Kila mtu anawajibika mbele za Mungu, kwa sababu tumeonywa mara nyingi kupitia kwa kurasa za kitabu hiki na zaidi sana kupitia kwa kurasa za neno lake takatifu. Onyo la neno lake latusababisha tukose sababu mbele zake.
Bibilia takatifu yaongea sana katika agano jipya kuhusu jehanamu, yataja kuzimu mara mia nne.
Yesu ni Mungu naye Mungu ni UPENDO. Lakini akirejea mara tena, atakuwa MFALME wa wafalme na BWANA wa mabwana na hakimu mwenye haki na mtakatifu.
Yesu akaniambia,”Onyo baada ya linguine limewafikia watu wangu, lakini wao hawa hawasikilizi, kulitii neno langu, wala kutilia maanani ufunuo zangu za sasa ambazo zimekuja kwa ajili ya ulinzi wao na upeanaji kwao. Kwa miaka mingi makanisa yamekuwa kimya na kuduwaa kwa mda mrefu na mara nyingi limeniach nje ya mipango zao.Sasa, nalifanya jambo jipya, name natumai kuwa watatubu na kunirudia sawa sawa na upendo wao wa kwanza, warejee kwa musingi ambao mimi mwenyewe niliujenga kulingana na kitabu cha matendo ya mitume, hata ninapo wainua mitume wapya, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu kutenda kazi katika huduma hizi tano kwaajili ya utukufu wangu. Kiwango chochote cha kiroho kisichoambatana na mambo haya ni uasi! Na kwa sababu uasi ni sawa na dhambi ya ushirikina, wale walio katika vyeo vilivyo na uasi, wamo katika hatari ya kuangamia kwenye ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti.
Mimi ni Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme katika vizazi vyote.

Tazama, naja upesi kama Mfalme wa mtakatifu na Hakimu wa haki.
Kwa hivyo, ni lazima uwaonye watu wangu!!!!"
Kabla Yesu kunituma nirudi kupitia kwa uwezo wa Roho mtakatifu, Aliniambia kuwa aliniruhusu nipitie haya mambo ili nijue kwamba haki yake ya siku za mwisho na onyo la siku za mwisho, anaitisha TOBA LA DUNIA NZIMA katika kila taifa!
Hili ni onyo kuu sana kwa makanisa na huduma zote katika mataifa yote.

*"Lakini Abrahamu akamjibu: Kumbuka mwanangu, kwamba ulipokea mema yako katika maisha, naye Lazaro akapokea mabaya. Sasa lakini, yeye anatulizwa, nawe unateswa. Licha ya hayo, kati yetu na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wanaotaka kuja kwenu kutoka huku wasiweze, wala wanaotaka kutoka kwenu kuja kwetu wasiweze." Luka 16: 26 – 27*

*" Kisha atawaambia wale walio upande wake wa kushoto, Ondokeni mbele yangu enyi mliolaaniwa! Nendeni katika moto wa milele aliotayarishiwa Ibilisi na malaika wake. Maana nilikuwa na njaa nanyi hamkunipa chakula; nilikuwa na kiu nanyi hamkunipa maji. Nilikuwa mgeni nanyi hamkunikaribisha; nilikuwa mgonjwa na mfungwa nanyi hamkuja kunitazama. Hapo nao watajibu, Bwana, ni lini tulikuona ukiwa na njaa au kiu, ukiwa mgeni au bila nguo, ukiwa mgonjwa au mfungwa, nasi hatukuja kukuhudumia? Naye atawajibu, Nawaambieni kweli, kila mlipokataa kumtendea mambo haya mmojawapo wa hawa wadogo, mlikataa kunitendea mimi. Basi, hawa watakwenda kwenye adhabu ya milele, lakini wale waadilifu watakwenda kwenye uzima wa milele." Mathaye 25: 41 - 46*

*" Basi, kama vile kila mtu hufa mara moja tu, kisha husimama mbele ya hukumu ya Mungu,…" Wahebrania 9: 27*

**SURA YA ISHIRINI NA MOJA**

**“NI KIPI KINACHO FUATA?”**

Nilikuwa katika mushtuko wakati  Roho Mtakatifu alinirejesha. Haikuwa rahisi kuamini kuwa nilikuwa nime pelekwa jehanamu, ingawa nilifahamu rohoni mwangu kuwa ilikuwa imetendeka kwa uwezo wa kiungu.
Nilikosa amani kwasababu nilikuwa nimeyapokea mengi sanausingizini kiaasi kwamba sikuweza kumwambia mume wangu chochote wakati huo.
Nakumbuka baadaye nilionekana mtulivu sana nilipomwelezea matembezi yangu kule Jehanamu nikiwa na Yesu. Uhakika way ale matembezi ukatuwa mawazoni mwangu. Kutokana na mapito hayo, Mungu aliyaondoa magamba kutoka machoni mwangu kimiujiza.
Huu ni ukweli kabisa kwasababu nilihisi katika Roho magamba yakitoka machoni mwangu. Mungu alikuwa amenionyesha ukweli ambao uliniweka huru kupitia kwa Kristo Yesu.

*“Mtaujua ukweli, nao ukweli utawapeni uhuru…………….. Kama mwana akiwapeni uhuru mtakuwa huru kweli.” Yohana 8:32, 36*

**SURA YA ISHIRINI NA MBILI**

**UHAKIKA WA JEHANAMU**

Siku illiyo fuata niliketi na mume wangu na tukaongea kwa md a mrefu na nikahisi tulizo kuu, ingawa mara yakwanza mume wangu alikuwa na mashaka kidogo kuyahusu mambo niliyo mwambia.
Niliondoka na kutembea polepole  huku nikinena kwa sauti ya chini nay a huzuninikisema," E Bwana, tazama haniamini kabisa, naomba kuwa umufungue moyo wake na macho yake ili auone ukweli."
Nilianza kuwa na wasiwasi kuhusunafsi nyingi zilizokuwa zikielekea jehanamu. Nami kikaanza kuuhisi musukumo kutoka ndani wa kushirikinna mtu mambo haya kwasababu sikutaka mtu yeyote aelekee kule.
Baada ya siku kadhaa, wakati wa jioni, nilianza kumwambia mume wangu kuhusu niliyoyaona kwa kuwa sikuwa na uhakika iwapo alikuwa ameshawishika kwa sababu, mda huu wote, alionekana wa machache. Hapo wote tukatambua kwamba alikuwa Mungu aliyekuwa anahakikisha kwamba tunakubali tukio hilo na lilikuwa limeruhusiwa naye.
Tangu wakati huo, kumekuwa na watu kadhaa ambao wamekuwa wakidhibitisha mambo haya. Nimenena na vigundi kadhaa, huduma kadhaa na baadhi ya makanisa. Mungu anataka achukuliwe kwa maanani.

Mda ni mfupi, na hili ni onyo kubwa sana kwa huduma, makanisa na mataifa yote kutubu!
Yale majira ya tarehe 17 Mei 2008, na zaidi ya miaka miwili, kwa mara nyingi nimahisi harufu ya kiberiti mapuani mwangu, masikio yangu yamesikia vilio vya nafsi zinavyo potelea kule jehanamu. Huu ni wakati ulio chaguliwa ya kuyaleta maono haya na kazi takatifu kuwa wazi kwa watu wa Mungu katika kila taifa ili watu wa Mungu waujue ukweli utakao waweka uhuru kwelikweli.

*"Nawaambieni hakika sivyo; lakini nanyi, hali kadhalika, msipotubu, mtaangamia kama wao." Luka 13: 3*

*"Tubuni, maana Ufalme wa mbinguni umekaribia." Mathayo 3: 2*

*"Nimeyafuta maovu yenu yaliyokuwa kama wingu zito, dhambi zenu kama dheluji. Nirudieni kwa kuwa nimewakomboa." Isaia 44:22*

*"Tazama, nitalitenda jambo jipya, nalo laja. Je, hamutaliona? Nitatengeneza njia jangwani na mito kwenye nchi kavu." Isaia 43: 19*

**SURA YA ISHIRINI NA TATU**

**MABADILIKO YALIYO TOKEA BAADAYE**

Nimesikia unabii mwingi sana kuhusu siku za mwisho ambao umehusisha Maono wazi wazi na ushuhuda wa malaika watakatifu kati yetu. Pia nimeziona nafsi zikiniomba msaada wakati ambao zina elekea kweny chombo cha hewa ilhali mimi sina uwezo wa kuzisaidia, hata Bwana Yesu hawezi kusaidia wakati huo manake washa chelewa.
Imehuzunisha roho yangu, name nimeugua juu ya mambo haya kwa mda, hasa nikitazama mambo yanayo endelea katika mwili wa Kristo zaidi sana Marikani. Roho yangu pamoja na hisia zangu zi makini kabisa, na kiwango cha upambanuzi kimeongezeka ndani mwangu kwa minajili ya utukufu wa Bwana. Kwa sababu yeye ana haja kabisa ya kuziokoa nafsi ili zisiangamie.
Naye Roho Mtakatifu amenipatia uwezo wa kupambanua mipango ya kipepo inayo endelea kule. Yesu Krito huniruhusu kujua nyakati ambazo yu karibu kutembea na kutenda jambo jinzi vile anavyo funia siri zake kwa watakatifu wake.

*"Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake." Amosi 3: 7*

Ninauona udanganyifu mwingi ambao shetani amepanda maishani mwa wale waliomokatika mwili wa Kristo. Yanaingiana moja kwa moja nay ale Yesu aliyo niambia tulipokuwa tukitembea.naomba kwamba utayafungua masikio yako ya rohoni na uyasikie na kutii kile ambacho Roho wa Mungu aishie anasema katika lisaa hili kwa wale walio salia siku hizi za mwisho ambao ndio Bibi harusi wa Mwokozi Yesu katika mataifa yote kabla hawajachelewa.
Ni heri umupokee na upokee mwito wake wa siku za mwisho ambao ameutoa kwa mataifa yote ya ulimwengu.

*"Na sasa, watoto wadogo, kaeni ndani yake, ili kusudi, atakapofunuliwa, mwe na ujasiri, wala msiaibike mbele zake katika kuja kwake."  Waraka wa kwanza wa Yohana 2: 28*

*"Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate. .............................................. Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?" Mathayo 16: 24, 26*

*"Lakini kama hamtaki kufanya neno hilo, ninyi mmefanya dhambi mbele za Bwana, nanyi jueni ya kwamba hiyo dhambi yenu itawapata hapana budi."  Hesabu 32: 23*

**SURA YA ISHIRINI NA NNE**

**FUNUO NA KWELI**

Funuo za kiungu ni: kwamba YESU KRISTO YU ARUDI UPESI! Tunavyo jua, mda unaisha. Hii yafananishwa na maji yaliyomo katikati ya vidole, na ni kwa uhitaji wa dharura kwamba jambo lisipo tendeka, yanakauka.

Bwana amemaanisha mno, naye hataki mtu awaye yeyote aende jehanamu. Lakini, iwapo mtu anachagua kuenda huko, basin i kutokana na dhambi ambazo hajazitubu. Hapo Bwana hatafanya chochote kumwokoa huyu mtu, kwasababu haya sii majira ya Mungu kupuuza dhambi za wanadamu bila adhabu kuu unayo kuja na hukumu.

Na maonyo mengi sana yataendelea kutoka vinywani mwa manabii wake (Mungu) , hivi karibuni itaanza na nyumba ya Bwana1 Bwana anatupenda wote na upendo usio na mipaka. Lakini hii haituruhusu sisi kuidhihaki kazi hii aliyo ikamilisha Kalivari. Kukanyagia damu takatifu ya Yesu Kristo kwa sababu ya dhambi ambazo hatujaitubu haitawezekana, kwasababu haruna kitu kama NEEMA YA GHARAMA YA CHINI katika ufalme wa Mungu.

Bwana anatamani wewe ujinyenyekeshe na umutafute kwa bidii kwanza, kasha uje kwake kila siku kwa toba katika Roho na ukweli. Toba yoyote isiyo na ukweli, yamufikia kama uvundo mapuani mwake.

Ni ukweli kwamba Yesu ni Upend, nan i wa rehema na neema. Lakini twafaa kuelewa kuwa, atakaporudi, atarudi kama mfalme na Hakimu.

*“Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi.*
*Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME, NA Bwana WA MABwana.” Ufunuo 19: 15 – 16*

Ninalijua jambo moja, kulingana na sura ya ishirini, kwamba Yesu alipoenda,alisimama akitazama kwa umakini, naye alikuwa na kitabu kikubwa kando yake. Yesu akanyosha mkono kuelekea kitabu naye akasema; “Hii ni taswira jinzi ninavyo kuja kuhukumu wote walio na mwili kulingana na matendo yao waliyo yatenda duniani kwa ukweli wangu kupitia kwa neno langu takatifu.”

Sio vyema kuambulia mikononi mwa Mungu aliye ghadhabika.

*“Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Wahebrania 4: 12*

**SURA YA ISHIRNI NA TANO**
**MAMLAKA YA BIBILIA JUU YA JEHANAMU**

Tafadhali enenda ukachukue bibilia yako takatifu, na ujitayarishe kupepea nami katika maandiko matakatifu.

1. **JEHANAMU NI YA KWELI NA NI MALALI HAKIKA**
   A. **ADHABU**

*“Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake;*
*na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi;*
*atawaweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto.*
*Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu;*
*kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha;*
*nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia.*
*Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha?*
*Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika?*
*Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia?*
*Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi.*
*Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake;*
*kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula; nalikuwa na kiu, msininyweshe;*
*nalikuwa mgeni, msinikaribishe; nalikuwa uchi, msinivike; nalikuwa mgonjwa, na kifungoni, msije kunitazama.*
*Ndipo hao pia watajibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au u uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie?*
*Naye atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea mimi.*
*Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.” Mathayo 25: 31 - 46*

   B. **ENENDA MOJA KWA MOJA HADI JEHANAMU NA NDANI YA MOTO.**

*“Na mkono wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili, na kwenda zako jehanum, kwenye moto usiozimika;*
*ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.*
*Na mguu wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima, u kiwete, kuliko kuwa na miguu miwili, na kutupwa katika jehanum;*
*ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.*
*Na jicho lako likikukosesha, ling'oe, ulitupe; ni afadhali kuingia katika ufalme wa Mungu, una chongo, kuliko kuwa na macho mawili, na kutupwa katika jehanum;*
*ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.” Marko 9: 43 – 48*

C. **AKIWA KUZIMU ALIYAINUA MACHO YAKE**

*"Akasema, Palikuwa na mtu mmoja, tajiri, aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, na kula sikuzote kwa anasa.*
*Na maskini mmoja, jina lake Lazaro, huwekwa mlangoni pake, ana vidonda vingi,*
*naye alikuwa akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka katika meza ya yule tajiri; hata mbwa wakaja wakamramba vidonda vyake.*
*Ikawa yule maskini alikufa, akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa, akazikwa.*
*Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na Lazaro kifuani mwake.*
*Akalia, akasema, Ee baba Ibrahimu, nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu.*
*Ibrahimu akasema, Mwanangu, kumbuka ya kwamba wewe uliyapokea mambo mema yako katika maisha yako, na Lazaro vivyo alipata mabaya; na sasa yeye yupo hapa anafarijiwa, na wewe unaumizwa.*
*Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze; wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu.*
*Akasema, Basi, baba, nakuomba, umtume nyumbani kwa baba yangu,*
*kwa kuwa ninao ndugu watano, ili awashuhudie, wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso.*
*Ibrahimu akasema, Wanao Musa na manabii; na wawasikilize wao.*
*Akasema, La, baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu.*
*Akamwambia, Wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu."*
*Luka 16: 19 - 31*

D. **NAFSI ZILIZO POTEA ZITAKUWA NA SEHEMU KATIKA BAHARI LA MOTO**
*"Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili." Ufunuo 21: 8*

E. **HATIMA YAKE NI ADHABU NA UHARIBIFU**
*"Hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia, na katika Akaya.*
*Maana kutoka kwenu neno la Mungu limevuma, si katika Makedonia na Akaya tu, ila na kila mahali imani yenu mliyo nayo kwa Mungu imeenea; hata hatuna haja sisi kunena lo lote.*
*Kwa kuwa wao wenyewe wanatangaza habari zetu, jinsi kulivyokuwa kuingia kwetu kwenu; na jinsi mlivyomgeukia Mungu mkaziacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli;" 1 Wathesalonike 1: 7 – 9*

2. **JEHANAMU NI MAHALI PA MATESO NA UCHUNGU WA MILELE**

A. **BAHARI LA MOTO**
*"Na majeshi yaliyo mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, safi. Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi."*
*Ufunuo 19: 14 -15*

B. **GIZA LA NJE**

*“Na mtumwa yule asiyefaa, mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.” Mathayo 25: 30*

C. **UHARIBIFU WA MILELE**

*“Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanum.” Mathayo 10: 28*

*“Kumcha Bwana ndio mwanzo wa hekima, Wote wafanyao hayo wana akili njema, Sifa zake zakaa milele.” Zaburi 111: 10*

*“Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima; Na kumjua Mtakatifu ni ufahamu.” Zaburi 9: 10*

D. **KULIA NA KUSAGA MENO**

*“bali wana wa ufalme watatupwa katika giza la nje, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.” Mathayo 8: 12*

E. **ADHABU YA MILELE**

*“Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.” Mathayo 25: 46*

F. **MAHALI PASIPO NA TUMAINI**

*“Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze; wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu.”Luka 16: 26*

3. **MAHALI PASIPO NA PUMZIKO MILELE**

A. **MATESO MILELE**

*“Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake.” Ufunuo 14: 11*

B. **MOTO USIOZIMWA**

*“Na jicho lako likikukosesha, ling'oe, ulitupe; ni afadhali kuingia katika ufalme wa Mungu, una chongo, kuliko kuwa na macho mawili, na kutupwa katika jehanum;*
*ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.” Marko 9: 47 – 48*

C. **MOTO WA MILELE**

*“Basi mkono wako au mguu wako ukikukosesha, ukate ukautupe mbali nawe; ni afadhali kuingia katika uzima hali umepungukiwa na mkono au mguu, kuliko kuwa na mikono miwili au miguu miwili, na kutupwa katika moto wa milele.” Mathayo 18: 8*

4. **JEHANAMU NI MAHALI PA WAKAAZI WABAYA NA WAOVU**

A. **SHETANI NA MALAIKA WAKE WALIO ANGUKA**

*“Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake;” Mathayo 25: 41*

B. **UOVU WOTE WA VIZAZI VYOTE**

*“Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje?*
*Na mwenye haki akiokoka kwa shida, yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi ataonekana wapi?” Wareka wa Petero wa kwanza 4: 17 – 18*

C. **KUTOTII**

*“na wale wenye fitina, wasioitii kweli, bali wakubalio dhuluma, watapata hasira na ghadhabu;*
*dhiki na shida juu ya kila nafsi ya mwanadamu atendaye uovu, Myahudi kwanza na Myunani pia;” Warumi 2: 8 – 9*

D. **WASIOAMINI NA WAONGO**

*“Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.” Ufunuo 21: 8*

E. **SODOMA NA GOMORA**

*“Kama vile Sodoma na Gomora na miji iliyokuwa kando-kando, waliofuata uasherati kwa jinsi moja na hawa, wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili, imewekwa kuwa dalili, wakiadhibiwa katika moto wa milele.” Yuda 7*
*Elekezi : Mwanzo 19: 1 – 29 na Warumi 1: 16 – 17*

5. **WASHIRIKI WA MWILI WA KRISTO WANAOKOSEA**

*“Kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu;........... Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza.” Petero wa pili 2: 4, 20*

6. **WALE AMBAO HAWAKUWAHI TII**

*“na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake*
*katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu;*
*watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;” 2 Wathesalonike 1: 7 – 9*

7. **YEYOTE ALIYEORODHESHWA JEHANAMU ATAISHI KULE MILELE**

*“Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi.” 1 Wakorintho 6: 9 – 10*

8. **ADHABU YA MILELE**

*“Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.” Mathayo 25: 46*

9. **UHARIBIFU WA MILELE**

*“Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanum.” Mathayo 10: 28*

10. **UHARIBIFU USIO NA MWISHO**

*“katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu;*
*watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;” 2 Wathesalonike 1: 8 – 9*

11. **HUKUMU WA MILELE**

*“na wa mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele.” Wahebrania 6: 2*

**SURA YA ISHIRINI NA SITA**

**MPAMGO KAMILI WA MUNGU**

1. **MUNGU ASHATENDA SEHEMU YAKE**

*“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*
*Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.” Yohana 3: 16 – 17*

2. **ALIDHIHIRISHA UPENDO WAKE**

*“Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.*
*Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye.” Warumi 5: 8 – 9*

3. **ALIMWAGA DAMU YAKE KWA AJILI YA WOTE**

*“Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;” Wakolosai 1: 13 – 14*

4. **HAKUNA ONDOLEO LA DHAMBI BILA UMWAGIKAJI WA DAMU**

*“Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo.” Wahebrania 9: 22*

5. **INJILI YAWEZA KUOKOA**

*“Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.” Warumi 1: 16*

6. **YAWAPASA WANADAMU KUSIKIA KUAMINI NA KULITII NENO**

*“Kwa hiyo wekeeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa roho zenu.” Yakobo 1: 21*

7. **WANADAMU WOTE WANAALIKWA**

*“Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.*
*Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu;*
*kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi.” Mathayo 11: 28 - 30*

8. **IMANI HUJA KWA KULISIKIA NENO LA MUNGU**

*“Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.” Warumi 10: 17*

9. **SIKILIZA NA UTENDE MAPENZI YA BABA**

*“Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba;*

*mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba." Mathayo 7: 24 – 25*
*"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni." Mathayo 7: 21*

10. **AMINI INJILI YA YESU KRISTO**

*"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao." Wahebrania 11: 6*

11. **IMEANDIKWA ILI UWEZE KUAMINI**

*""Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki.*
*Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake." Yohana 20: 30 – 31*
*"Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu." 1 Waraka wa Yohana 5: 13*

12. **UTUBU AU UANGAMIE**

*"Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu." Luka 13: 3*
*"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa." Marko 16: 16*

13. **TUMEAMURISHWA KUTUBU**

*"Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu." Matendo 17: 30*

14. **MKIRI YESU KRISTO MBELE YA WANADAMU**

*"Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni.*
*Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni." Mathayo 10: 32 – 33*
*"Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu;" 1 Temetheo 2: 5*

15. **MUKIRI YESU KRISTO KWA KINYWA CHAKO**

*"Kwa maana neno la ahadi ni hili, Panapo wakati huu nitakuja, na Sara atakuwa na mwana.*
*Wala si hivyo tu, lakini Rebeka naye, akiisha kuchukua mimba kwa mume mmoja, naye ni Isaka, baba yetu," Warumi 9: 9 – 10*

16. **UBATIZWE KWA SABABU YA ONDOLEO LA DHAMBI**

*"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Matendo 2: 38*

17. **BATIZWA ILI UOKOKE**

*"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa." Marko 16: 16*

18. **BWANA ANATUONGEZA KWA KANISA LAKE**

*"wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." Matendo 2: 47*

19. **IWENI WAAMINIFU HATA KWA MAUTI**

*Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima." Ufunuo 2:* 10

*"Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa." Ufunuo 12: 11*

20. **VUMILIA HADI MWISHO**

*"Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka." Mathayo 10: 22*

*"Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu." Mathayo 5: 11*

*"Yesu akawajibu, Je! Mnasadiki sasa?" Yohana 16:31*

21. **IWENI IMARA, BILA KUSUKUMWA NA MAKUBALIANO**

*"Basi, ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana." 1 Wakorintho 15:58*

**SURA YA ISHIRINI NA SABA**

**NENO LA UFUNUA LA ROHO MTAKATIFU KUHUSU BI HARUSI WA BWANA YESU KRISTO TAREHE : 6/ 2 / 2010**

Neno hili la ufunuo wa Roho Mtakatifu lilimjia ovasia wetu ambaye ni mtume wa Kristo, jina lake ni ndugu Patrick A. Kirk, tarehe sita Februari 2010 saa saba za asubuhi, kama wajibu takatifu wa makanisa na huduma zote katika mataifa yote kwa ajili ya ufakme wa Mungu na kwa utukufu wake;
"Kanisa la karne ya kwanza kulingana na tangazo la Yesu kwamba" wala hawatasema, Tazama, upo huku, au, kule, kwa maana, tazama, ufalme wa Mungu umo ndani yenu."(Luka 17: 21) unatenda kama ufalme ndani ya mpangilio wa kiungu wa ufalme ambao msingi wake uliwekwa na kuzimikwa na Yesu mwenyewe, unahusihsa: (1) Mitume; (2) Wainjilisti; (3) Manabii; (4) Wachungaji; (5) na Walimu. Hii ni sawa sawa na Waefeso 4: 11 – 16; Waefeso 1: 1 – 23; na Warumi 1: 9 – 12.
Iwapo haya matawi matano ya huduma na mpangilio wa kibibilia ulio wa kiungu ambao waenenda hivi: Mitume, Manabii, Wainjilisti, Wachungaji na Walimu hautakubaliwa na kukumbatiwa makanisani na katika huduma leo, bas litakuwa dhihirisho la uasi kinyume na Mfalme wa wafalme na mpangilio wake wa kiungu katika siku hizi.
Kukubali mpangilio huu wa kiungu kikamilifu wahitaji makanisa ya msingi na huduma zote kukubali gharama hizi tano kutenda kazi kupitia kwa Roho wa Mungu aishiye kwa niaba ya mahitaji ya washirika walio katika makubaliano na Waefeso 4: 16.
Iwapo makanisa na huduma zitakataa kuruhusu gharama hizi kutenda kazi (Kama zilivyo tenda kwa karne ya kwanza), basi yamaanisha kwamba makanisa na huduma zimo katika uasi kinyume na Mungu na kinyume na mpangilio wake wa kiungu katika ufalme siku hizi tulizomo. Na kwa ukosefu wa toba ya kweli , chaguo lilipo kwa makanisa haya na huduma hizi ni adhabu ya Mungu na hukumu!
Tafadhali, nawasihi kwamba tukumbuke kuwa machoni mwa Mungu, UASI WOTE ni ulogi au uchawi na kwahivyo ni chukizo mbele za Mungu, kulingana na Medhali 6: 16 – 19!
Uasi ni chanzo cha dhambi zote.
Sasa hivi tumo katika kizazi cha ufalme wa Mungu Mwenyezi na mwanawe mpendwa, Yesu Kristo. Nasi sote basi twahusu kazi ya Baba wetu wa mbinguni anaye penda nafsi zote na kuchukia dhambi zote.
Pia yatupassa tuwe na nia ya ufalme moyo wa kweli wa ufalme unaofanana na wa Baba yetu aliiye mbinguni, ambayo itatuweka katika hatua za mpangilio wa Mungu wa siku za mwisho, Makusudi yake na hatma yetu tuliomo katika ufalme wake leo.
Tafadhali soma kitabu cha Mika 3:1 – 12 na Malaki 3: 1 – 11!
HUKUMU Utaanzia nyumbani mwa Mungu katika lisaa tulilomo!
Manabii wanao julikana vyema marekani watakuwa wa kwanza kuhukumiwa kwasababu wanatumikia roho za fedha, ulafi, na ushawishi mbovu.
Mungu anachukia mambo haya, na hivi karibuni hukumu wake anawadia.
Mungu mwenyezi yu karibu kudhibitisha musimamo wake wa kiungu kwetu (Makanisani na katika huduma za leo), mara tena kwa urejeo mtakatifu kwa adhabu na hukumu, sawa na vile ilivyokuwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume sura ya tano. Aliwaita na kuwaadhibu watu wake kwa kutenda dhambi kinyume na Roho Mtakatifu.
Kwa hivyo enyi watakatifu wapendwa, yatupasa kutubu kabla hatuja chelewa!"
Katika huduma wa upendo wa kwa Mungu na mwanawe Yesu Kristo katika mataifa yote, Ninabaki katika Kristo Yesu, Mtume Patrick A. Kirk (Mtumishi kwa watumishi)

## SURA YA ISHIRINI NA NANE

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nakili**

“KUKOMBOLEWA KUTOKA JEHANAMU ”kwamaanisha vile vile. Kuna baadhi ya vitu vinavyohitajika ili mtu aondoke au asalie jehanamu jinzi nilivyo onyeshwa na Bwana Yesu

1. TUBU dhambi zako zote katika masaa ishirini nan ne
2. UTAKATIFU: anza kuyaishi maisha matakatifu kanakwamba wamuishia Bwana. Kama wakristo tumesahau kufanya hivyo kabisa.
3. UWEMNYENYEKEVU: (Iwapo unaweza kudhihirisha katika asli), lala kifudifudi mbele za Bwana na umtafuteMungu katika upweke wako kupitia kwa mwanawe Yesu Kristo. Inama mbele za uwepo wake kama ishara ya kujinyenyekesha kwa mkono wake wa kiume ulio na nguvu na mamlaka.
4. KILA SIKU KUREJELEA UPENDO WAKO WA KWANZA KWA YESU; Na umudhamini , tunapomtumikia mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, sio kama rafiki wa awali – kwasababu Yesu yu aja upesi kama hakimu mwenye haki.
   *“baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.” 2 Temetheo 4: 8*

   *“mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika,.............. maana Mungu wetu ni moto ulao.” Wahebrania 12:23, 29*

   *“kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu.” 1 Petero 4: 10*

   *kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu.” 1 Petero 1: 16*

   *“Bali mimi nawaambieni, Kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu; na mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza; na mtu akimwapiza, itampasa jehanum ya moto.” Mathayo 5: 22*

   *“Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.” Mathayo 6: 14 – 15*

   *“Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake.” Warumi 13: 14*

   **UNYENYEKEVU**

   Kila mmoja wetu anafaa kujichunguza na kasha tuyaweke maisha yetu na mtembeo wetu wa kila siku kuwa sawa na Yesu Kristo ili aendelee kutusafisha nasi tufanywe watakatifu nyakati zote mbele za Bwana. Tuna faa kutubu na kuachana na kila aina ya kutosamehe (kisasi).
   Tutubu na tuachane na kila aina ya kiburi. Tuachane na kila aina ya vinyago na kuabudu sanamu kama; hela, milki na hata wanadamu.
   Mtu au kitu chochote ambacho huchukua nafasi ya kwanza maishi bila shaka hufanyika mungu kwa mtu huyo.
   Vitu ivyo ndivyo ambavyo Mungu haviruhusu katika ufalme wa mbinguni. Vitu kama usinzi, ulawiti, ulafi ushawishi mbaya, kupenda fedha na aina yote ya uasi kinyume na Mungu mwenyezi

ni vitu ambavyo Mungu ametangaza kwamba vitaipeleka nafsi jehanamu kwa chaguo la mtu mwenyewe.
Tumepotoka na kuenenda kwa njia zetu wenyewe kwa mda mrefu! Katika Zaburi 46: 10, Bwana asema, "Simama wima nawe utajua kuwa mimi ni Mungu."
*"Bali maneno yenu yawe Ndiyo, ndiyo; Siyo, siyo; kwa kuwa yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu." Mathayo 5: 37*

*"Kumcha Bwana ni kuchukia uovu; Kiburi na majivuno, na njia mbovu, Na kinywa cha ukaidi pia nakichukia." Medhali 8: 13*

*"Lakini hutujalia sisi neema iliyozidi; kwa hiyo husema, Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu. Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia." Yakobo 4: 6 - 7*

*"Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele." Wagalatia 6: 7 – 8*

**SWALI LA KWANZA**
Baadhi ya watu wameuliza, "iwapo Bwana antaka watu wafahamu haya, na watu walemavu je?" Neno lasema ndiyo. Kila mmoja atajua
*"Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia. Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru;" Warumi 1: 19 – 20*

**SWALI LA PILI**
Je haya yalikuwa maono ama kitu kingine?
Mimi, Bette Stevens niligeushwa na Roho Mtakatifu, Yesu Kristo akiwa kando yangu name nikaenda hadi kule jehanamu. Naye Roho akaniwezesha na roho yangu na katika hisia zangu kufahamu kila kitu kilichokuwa kikitendeka. Niliona, nikasikia na nikahisi kla kitu ambcho kimenakiliwa kitabuni humu kulingana na kile Mungu aliniwezesha kukiona katika ile safari ya kuzimu. Tangu siku hiyo, nimekuwa na maono ya wazi kabisa nikizion anafsi zikiteremka na kuingia jehanamu katika shomo livutalo. Kila mara nimesikia vilio vyao na sauti zao zikiita na kusema, "nisaidie! Sikujua nitakuja hapa ni heri mtu angeniambia!"
Jawabu timamu la hili swali," Kwanini sikuambiwa na mtu?" ni kwamba kwa vizazi vingi sana, uasi umetawala mioyoni mwa watu wa Mungu; nao wameshindwa kutoa maonyo yaliyo sawa na mwito kwamba kunayo mbingu ambayo watu wanafaa kuingia na jehanamu ambayo watu wanafaa kuitoroka.! Yesu Kristo atamuuliza kila mukristo maswali kuhusu jambo hili hiyo siku akiwa katika kiti kikuu cheupe cha hukumu.
*"Basi wewe, mwanadamu, nimekuweka kuwa mlinzi kwa nyumba ya Israeli; basi ulisikie neno hili kinywani mwangu, ukawape maonyo yangu. Nimwambiapo mtu mbaya, Ewe mtu mbaya, hakika utakufa, nawe husemi neno la kumwonya mtu huyo, aiache njia yake, mtu mbaya huyo atakufa katika uovu wake, lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Walakini ukimwonya mtu mbaya kwa sababu ya njia yake, kusudi aiache; wala yeye asiiache; atakufa huyo katika uovu wake, lakini wewe umejiokoa roho yako." Ezekieli 33: 7 – 9*

**SWALI LA TATU**

"Wewe u aje? Kuna otofauti wowote ndani yako?"

Bila shak ndiyo, mimi humtafuta Bwana kila siku kwa sifa na kuabudu na toba ya kila siku! Maono mengi sana ya kinabii yamenijia. Ono lile ambalo ni la juzi kabisa ni lile ambalo Yesu kupitia kwa Roho Mtakatifu alinibadilisha na kunipepeka kwenye choomba cha enzi ya Mungu.ilikuwa tarehe 15/ 12/ 2010. Nilisimama mbele zake na huku Yesu amesimama katika utukufu wake akiwa na upanga ukatao kuwili! Kwa upole akasema, "Nabii, fanya ono hili kuwa juhudi iliyo wazi; liandike chini kasha ufanye watu wangu walifahamu. Lifanye liwe wazi kabisa kwao." Nimesikia juhudi hii takatifu marakadhaa.

*"Bwana akanijibu, akasema, Iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji. Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia." Habakuki 2: 2 - 3*

Jinzi vile nilivyo eleza mapema,tangu matukio haya, upambanuzi wangu umekuwa makini sana kupitia kwa uwezo wa Roho mtakatifu.

Maono ya wazi wazi na funuo za Roho mtakatifu zime dhibitishwa kwa kutimia. Sawa na vile nilipelekwa hadi chumbani mwa Enzi ya Mungu.

Maonyo ya kinabii ya mwisho wa nyakati, mwito na wajibu kila mara vimenijia kutoka rohoni. Naye Bwana amenidhibitishai kwamba vitu hivi vyote vyaja kutimia wala havitakawia hasa kwa taifa letu la Marekani.

**SWALI LA NNE**

"Je watu hawa ni waumini walio okoka au pengine ni wakafiri?"

Hakika, wote walikuwa wameokoka, na wengine hawakuwa wameokoka.

Lakini nafsi hizi nyingi zilizomjua Mungu zilikuwa zikimtumikia na tena zilikuwa na uhusiano wa karibu na Yesu. Lakini dhambi ziliingia maishani mwao na kwa chaguo lao wenyewe wakafanya uamuzi mbaya na wakakubaliana . watu hawa, wengi walikuwa na vyeo makanisani njia ya kwenda jehanamu imetengenezwa kwa upana kwa makusudi."ingia kwenye lango lililo nyooka, kwa kuwa lango pana , laelekea kwa uharibifu, nan i wengi wanaolipitia. Lakini lango jebamba laingia uzimani, nao ni wachache wanao liingia."

*" Je! Mwadhani ya kwamba nimekuja kuleta amani duniani? Nawaambia, La, sivyo, bali mafarakano." Luka 12: 51*

Je ninajuta kwa kupeana maisha yangu yte kwa Yesu na kumruhusu kuniongoza, kunielekeza na kunionyesha njia, hasa kwa gharama inayotokana na haya yote? La hasha, nimesema hivi, nimepeanwa kwake hata kwa kiwango cha kufa. Hakuna chochote kilicho chema kinachozidi kumtumikia Mungu. Dhawabu ni na litakuwa kuu kule mbunguni kuliko kila kitu chochote ambacho tungekipata hapa duniani.

*"Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa." Ufunuo 12: 11*

**SURA YA ISHIRINI NA TISA**

**"UDHARURA WA ONO"**

Nime lia mara nyingi na kila mara nimeugua katika roho yangu ninapoona katika Roho nafsi nyingi zinazo tumbukia katika moto wa jehanamu wa milele, pengine ni kwasababu ya kukosa kufahamu dhamu ambazo hazija tubiwa ndani mwao ambazo zimewanyima mbingu.
Udhrura wa Roho Mtakatifu ni mkuu sana! Bwana yu aniambia kusisitiza jambo hili zaidi.
Bwana ametoa maonyo mengi yakifuatana kupitia kwa manabii wake akiweka wazi neema na rehema zake, lakini watu wengi katika mwisho wa nyakati nyakati huu ambao bi harusi wa Bwana Yesu Kristo aandaliwa katika mataifa yote bado hawatilii maanani.

Hakuna mtu awae yeyote awezae kutoa hukumu ulio sawa isipo kuwa Bwana Mungu mwenyewe. Bali mimi nawalilieni na kuwasihi kwa upendo wa Mungu na kwa nguvu zake kwamba enyi mataifa yote mpate kutwaa juhudi hii ya onyo la mwisho kwa sababu hatima zetu za kiroho zaning'inia katika mizani katika lisaa hili!
Ee Mungu, zirehemu nafsi zetu!
Ni heri niwaone watu wakifanya juhudi za kufikia toba ya kweli na wawe na kicho kitakatifu cha Mungu Mwenyezi kabla hawajachelewa.

Bwana asema, "Iweke iwe wazi kwa watu wangu", sitaki nirejee (nije) kinyume na makanisa, kwa sababu vita vyetu ni kinyume ne mamlaka na nguvu za giza katika anga. Na kwa sababu yay ale nimeyaona juu ya makanisa katika Nyanja za rohoni,, ambacho ni kifukiko cha uoga, mashaka na kutoamini na uongo uliowekwa na shetani, watu wote lazima wafahamu kuwa Bwana ni hakimu mwenye haki, naye anaenda kunza kuhukumu huku akianza na nyumba ya Mungu ambalo ni kanisa.
Kama wachungaji na viongozi wa makanisa yatupasa tuanze kuhubiri, kufundusha, kuongea na kutembea huku tukilitenda neno la Mungu kikamilifu bila kuondoa sehemu ya maandiko eti kwa sababu "tutamuudhi mtu" au pengine kwamba "huenda ukapoteza baadhi ya washirika" ambao ndio husimama na huduma sana hasa kwa upande wa fedha au pengine wewe mwenyewe waona "si vyema kuongea juu ya mambo yaha." Bwana asema, "wacha kumzima Roho wangu, nawe uoeane neno kamili kwa utakatifu."

Bibilia yasema, *"Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki." Ufunuo 22: 18 - 19*

Mungu hadhihakiwi: chochote upandacho, ndicho utakacho kivuna!
"Akawaita mkutano pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, Mtu ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike na msalaba wake, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha. Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake? Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake?
Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu, katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu." Marko 8: 34 - 38

## SURA YA THELATHNI

## KUSONGA MBELE

Hivi ndivyo mabo yalivyo, sikuwahi fikiri kuwa ningeketi china siku moja na kuandika maonyo ya kinabii, ila Bwana ameitangaza! Nimeandika nab ado nitaendelea kuyanakili yale Ambato Bwana atanieleza! Bwana yu atenda jambo jipya! Kunao upako mpya na mtakatifu ambao waja, hat anapo waita wanawe wa hizi siku za mwisho kurejea katika msingi wao wa kwanza, uliowekwa na Yesu Kristo katika karne ya kwanza. Kwasababu kando na mambo yote, kunao walio saliaambao bado wamesimama, wale wanao ujua ukweli wa Mungu katika lisaa hili,kwamba hakuta kuwa na makubalianoyoyote na dhambi, ila toba. Huu ni mwito wa Bwana ulio wa mwisho katika huu mwish wa nyakati, kwa watu wote katika mataifa yote!

Yesu asema,"Njoni kwangu upesi kwa toba kamili. Mimi ni Mungu mwenye wivu. Yatende mambo muliyo yatende hapo mwanzoni. Ninawaamuru muwe na utiifu, utakatifu, Uaminifu, toba, haki, na ushikamako kwa neno la Mungu! " Asema Bwana wa majeshi.

Ilinipasa nimngoje Bwana ili ujumbe huu utokao moyoni mwake udondoke moyoni mwangu kikamilifu. Kwa nini? Ni kwa sababu kilakitu hufanyika sawa iwapo kimo katika wakati sawa wa Mungu na katika mapenzi yake kamili kwa nyakati kama hizi!

Kunayo maonyo mengi na hukumu zinazo kuja. Zitakuja kwa mkazo kitaratibu katika siku zijazo!

Ni wakati wa watu wa Mungu kuujua ukweli wa Mungu. Kwa sababu usipojua, hakuna njia mbadala wala msaada mwingine. Wakati wa kubadilisha hukumu ni sasa,.

Hata ninapoiandika surah hii ya mwisho Bwana yu ainua mitume na manabii wake na walinzi kutoa mwito wa mwisho na kutanguliza baragumu ya wito na wajibu takatifu la kutubu!

Watu wa Mungu wengi sana wanalala kwa haraka, nao wana starehe, ilhali mambo ni tofauti sana "kule kwingine ambako ni jehanamu." Mda unakwisha, na jehanamu ni hakika ipo milele!

Ningependa kusema tena kuwa, jehanamu ipo na ina inaendelea na kufuliliza; na hakuna kuhepa huko. Pengine waweza kusema kuwa hii ni kuuonyesha uchungu mzito mno. Ndiyo, huwo ni ukweli, lakini ni heri kueleza hivi kuliko kupoteza nafsi yako kule jehanamu.

Mwili wa Kristo wafaa kuwa tayari kwasababu tunaenda kuadhiriwa na matukio ya mwisho wa nyakari yanapo dhihirika. tunahitaji neno la Mungu la kweli na ushauri kamili wa neno la Mungu na mafundisho yaliyo sawa yakiambatana na uhusiano wa ndani wa Kristo Yesu.

Shauku langu kuu ni kuziona mamilioni za nafsi zikija kwa Yesu na kumpokea kama Bwana na Mwokozi, masia, mfalme na hakimu kabla hazijachelewa.

Ninatamani kuziona zikiingia mbinguni nan a zingine ziki chomolewa kabla ziingie jehanamu!

Wajibu wa kitabu hiki ni kuwachochea watu wa Mungu kwa sababu sitaki damu ya mtu yeyote ihesabike juu ya kichwa change wala mikono yangu.

Wala sitaki kusimama mbele za Mungu na hatia ya damu ya mtu mikononi mwangu eti kwa sababu niliogopa kunena kwa ujaziri wake mtakatifu ili kumuonya bi harusi wa Bwana ayesu Kristo kutoka kwa kila taifa kuhusu hukumu wa haki wa Mungu unao subirikuja.

Yesu yu atafuta majeshi wake watakatifu wa ufalme wake. Yeye yu ajitwalia jeshi lake la nyakati za mwisho ili kufuliliza hadi kwa utukufu wake.

Ningependa kumalizia kwa kuliza swali hili: "JE, UTASIMAMA WAPI KWA UMULELE WAKO"

Je, utasimama kwenye sehemu ya moshi (Jehanamu)? au utasimama pale pasipo na moshi (Mbinguni)?

*"Maana twamjua yeye aliyesema, Kupatiliza kisasi ni juu yangu, mimi nitalipa. Na tena, Bwana atawahukumu watu wake.*

*Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai." Wahebrania 10: 30 - 31*

Ninaamini kuwa sasa waelewa kuwa hela na vitu vyote vya dunia hii yakiwemo “matendo mema” havina uwezo wa  kukupeleka mbinguni wala kukuongezea mda duniani.
Hakuna kutokuwa moto au baridi, kufanya sarakasi na mzaha mbele za Mungu. Mungu ni hakimu mwenye haki na ufalme wake umewadia.
*“Naye heri mtu ye yote asiyechukizwa nami” Luka 7: 23*
Kwa ukuu, Mungu anainua Mitume, Manabii, Wainjilisti, Wachungaji na Walimu watakao simama hizi siku za mwisho.
Halija wahi badilika kutoka Mwanzo hadi ufunuo: *“Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele.” Wahebrania 13: 8*
Wanadamu walilibadilisha neno hili; kwa hivyo, Mungu yu ainua Bi harusi aliye salia wa Kristo katika kila taifa kurejea kwa utendaji katika msingi wa Yesu Kristo mwenyewe kwa makanisa na huduma zote duniani kupitia kwa gharama tano za huduma  wake zikidhihirika kwa minajili ya kuwavika watakatifu wa Mungu.
Ninawaombea ndugu na dada zangu wote wakiwemo wale ambao wameokoka na wale ambao wamepotoka kutoka kwa njia za Mungu! Tafadhali ninawasihi njoo, tubu na mrejee kwa Mungu wa kweli kupitia kwa Bwana Yesu Kristo!

**VICTORIOUS VISION MINISTRIES, INTERNATIONAL; LLC.**

Iwapo wataka kupata habari zaidi kuhusu huduma wa Kristo Yesu kati yetu;iwapo wahitaji maombi yoyote, Ushauri, Ukombozi, kuelekezwa katika haki ama pengine wahitaji mahali pa kuabudu na kushiriki, tafadhali tazama tuvitu ya huduma wetu:
http://www.shoutlife.com/victoriousvision AU
http://www.vvmint.webs.com
Pia waweza kutufikia kupitia sanduku la posta: Victorious Vision Ministries International; LLC.
P.M.B. # 232
1933 East Dublin-Granville Road
Columbus, OH 43229-3508.

Agosti 2010, pia tume toa “CD” ya maongezi iitwayo: “THE CLARION CALL OF 2010!” na pia tumechapisha shajara ya huduma, pia inapatikana. Tafadhali wasiliana nasi.
Medhali 10: 22 na Hesabu 6: 24 - 26

**KWA UFUPI**

Bwana hataki mtu yeyote aangamie, kwa sababu anao upendo mkuu kwako na kwa wanadamu wote kwa jumla.
*“Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.” Yohana 3: 16 - 17*

Ni shauku lake la milele kuwa wewe uwe na uhusiano wa kweli, wa karibu na wa ndani na Yesu Kristo, kwa kuwa yeye ndiye Bwana harusi, ambaye hivi karibuni yu aja kumtwaa Bi harusi asiye na waa lolote wala kunyanzi, ambaye vazi lake la harusi limeoshwa na kusafishwa kwa damu ya Mwana Kondoo wa Mungu.
Ninawaombeeni enyi watakatifu wapendwa wa Mungu, na ninawapenda wote kwa upendo wa Kristo, TAFADHALI, musingoje, yaweke maisha yenu sawa na Bwana Mungu wetu!!
IWENI TAYARI SIKU ZOTE!!!!

**KUHUSU MWANDISHI**

Bette Stevens anaishi na mumewe, John, kule Kolombia, Ohio.
Yeye pamoja na mumewe walizaliwa na kulelewa huko. Wanao watoto wanne ambao tayari ni watu wazima, na wana wajukuu kumi nan ne.
Mumewe John ni mchungaji/ Muinjilisti. Wao husafiri pamoja wakihudumu na bila shaka wana karibisha mwaliko wako kuja kuhudumu kanisani mwako ama kwa mikusanyiko yoyoyte ya kikristo.
Bette na John wamekuwa viongozi katika kanisa lao la nyumbani, wametenda kazi katika ghala la chakula na kufanya uinjilisti kwa ujirani na pia wametumika kuunganisha watu na huduma kukiwepo na uhitaji. Wamebeba shauku la kweli la Yesu Kristo kwa ufalme wake hizi siku za mwisho kwa mataifa yote.

**KUMHUSU OVASIA WETU NA MTUME PARICK A KIRK (Mtumishi kwa watumishi)**
**KINGDOM ENCOURAGERS MINISTRIES & CHURCHES, INTERNATIONAL, LLC. :**

**“KWA UTUKUFU WA MUNGU NA KWA KUMTAYARISHA BI HARUSI KATIKA MATAIFA YOTE”**

Wajibu na maono ambayo Mungu alitupatia katika huduma na makanisa ya “Kingdom Encouragers” ni kwamba tuwe watiifu kwa MWITO KUU kutoka kwa Yesu, jinzi ilivyo katika: Matayo 28:18-20; Marko 16:15-16; 1 Wakorinthο 13:1-13 na Wagalatia 5:22-24

Tunaamini kuwa Yesu Kristo ndiye kiongozi mkuu wa Bi harusi Kristo wa waumini wa ufalme wote.

Tumaamini katika ubatizo kamilifu wa Roho Mtakatifu na katika mpangilio asli wa ufalme na msingi wa kiungu ambao Yesu Kristo mwenyewe aliuzimika katika kanisa lake la karne ya kwanza likiwa na gharama tano za huduma zikitenda kazi kikamilifu zikiwemo: Mitume, Nabii, Muinjilisti, Mchungaji na Mwalimu. Ambapo kila tawi lilitenda kulingana na Waefeso 4:11 – 16, Waefeso 1: 1 – 23, Warumi 1: 9 – 12

Mungu ataka watakatifu wake wa ufalme waandaliwe ya kutoshana wafundishwe na wajazwe na Roho Mtakatifu kutoka mbinguni kwa ukamilifu wa Mungu kupitia kwa Kristo Yesu

Ili kanisa liwe tayari kwa kazi ya ushindi kwa ajili ya utukufu wake. Maisha katika Kristo Yesu yadhihirika vyema kupitia kwa Roho Mtakatifu aliymo ndani yetu. Akitupatia hakikisho la kweli kuhusu uwepo wa Mungu, Nguvu, utakatifu, upako na utukufu uliomo katika watakatifu wake.

Tunaamini na kutenda katika mtazamo wa Mungu wa isaha, miujiza na maajabu inayo dhihirika kupitia kwa mitume waliomo kati yetu na utendaji wa gharama zingine zote tano.

Kwa shauku iliyo kuu na unyenyekevu, Mungu anita watu: 1) Toba ya kweli ulimwengu mzima; kwa makanisa yoto na huduma katika kila taifa. 2) Kumurejelea Yesu kikamilifu akiwa mpenzi wetu wa kwanza na turejee kuyatenda mambo tuliyo kuwa tukiyatenda katika upendo wetu wa kwanza. 3) Kurejelea mpangilio takatifu ulio wekwa na Bwana Yesu katika kanisa la karne ya kwanza. Makanisa na huduma zinazo kubali na kukumbation utendaji wa gharama hizi tano yatapanuka na kubarikiwa.

Nayo makanisa yanayokataa yatagwama njiani na kuambulia jehanamu.

Kukataa kurejea kwa mpangilio wa Yesu wa kwanza ni kukuwa katika uasi kinyume na juhudi ya lisaa hili. Uasi ndio chanzo cha kila dhambi. Mungu anachukia uasi kwa sababu ni kama dhambi za Uchawi na ushirikina. Na tna ni chukizo mbele ya Mwenyezi Mungu. Tazama Medhali 6: 16-19

YESU KRISTO ndiye mtume mkuu anaye fundisha mataifa yote na vizazi vyote. Naye ndiye Kiongozi wa kweli aliye mkuu wa kanisa laeo na hata milele.

Tunakuhimiza kutualika tuje kuhubiri na kufundisha kanisani mwako, kwa huduma wako au kikundi chanu cha kikristo.

Ninawahimiza kutazama tuvuti yetu ya huduma:

Tuvuti ya huduma: http://www.shoutlife.com/keminschurchesintl
Barua pepe : patrick.kirk1947@yahoo.com
Simu: 1-614-396-6774
Sanduku la posta: Kingdom Encouragers Ministries & Churches, Int’l, LLC.
Apostle Patrick A.Kirk
P.M.B. # 231 1933 East Dublin-Granville Road
Columbus, OH 43229-3508.

Katika huduma wa Munguna kwa wana wa Mungu wote katika Bi harusi wa Kristo Yesu aliyesalia katika mwisho wa nyakati katika mataifa yote, Ninabaki wenu,

Mtume Patrick A. Kirk